SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



RIPOTI MAALUM
**Zebaki** ilivyobeba sumu kwa ujauzito hadi mazingira
UK. 4


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Oktoba 24, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • No. 0580743

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




**Shilole** wapashe wapashike
UKURASA 20

# Giza nene mradi stendi ya Mwenge

UKURASA 2



Mwonekano tofauti wa majengo ya mradi wa stendi mpya ya mabasi Mwenge, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, ambao ujenzi wake, unaonekana kusuasua. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Ndugai aonya wabunge kuitwa mazuzu

UKURASA 3



## Samia apata dawa ya ukatili

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA, JWANENG KUMALIZA UBISHI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Samia apata dawa kukomesha ukatili

**Na Julieth Mkireri,** RUFIJI

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka wanawake kuungana kupinga ukatili unaofanywa dhidi yao.

Alitoa rai hiyo jana alipohutubia kwenye maadhimisho ya kilele cha Wiki ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) yaliyofanyika Ikwiriri wilayani Rufiji mkoani Pwani jana.

Alisema lipo ongezeko la vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake ambapo wanawake wamekuwa hawapazi sauti ipasavyo kukomesha vitendo hivyo.

"Ninadhani wanawake tunachangia kwa sababu linapotokea tunalikingia kifua, haipendezi kukuta mwanamke mwenzio anadhalilishwa nawe ukasimama kulitetea kwa sababu aliyefanya kitendo hicho ni ndugu au kaka yako," alionya.

Rais aliwataka wanawake kubadilika na kusema yale yaliyo mazuri na kuacha na kusemeana mambo ya uongo, wapendane na kushirikiana katika kumkomboa mwanamke kiuchumi na kifikra.

Rais Samia pia alitoa rai kwa watafiti na waandishi wa sayansi ya historia kuandika kuhusu Bibi Titi Mohamed.

"Wangapi wana ujasiri wa kuwaunganisha wanawake wa Kitanzania kupata ukombozi wa kifikra? Tunatakiwa kuyaenzi yale yaliyofanywa na Mwenyekiti wa kwanza wa UWT, Bibi Titi Mohamed," alisema.

Mwenyekiti wa UWT Taifa, Gaudensia Kabaka, aliwataka wanawake kumpa ushirikiano Rais Samia katika utekelezaji wa majukumu yake ili kupata matokeo ya haraka.

Katibu Mkuu wa UWT, Phills Nyimbi, alisema jumuiya hiyo inampongeza Rais kwa kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati na utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge, alimshukuru Rais Samia kwa kutenga fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika mkoa huo.

Kunenga alisema serikali imetoa Sh. bilion 21 kwa ajili ya miradi ya maji inayotekelezwa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Pia alishukuru ongezeko la bajeti ya barabara za mjini na vijijini kutoka Sh. bilioni tisa mwaka 2020/21 hadi Sh. bilioni 43 mwaka huu.

Mbunge wa Rufiji, Mohamed Mchengerwa, alipongeza jumuiya hiyo kufanya maadhimisho hayo katika jimbo hilo na kujenga mnara wa kumuenzi Bibi Titi Mohamed.




Rais Samia Suluhu Hassan, akihutubia katika maadhimisho ya Kilele cha Wiki ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), iliyoambatana na kumbukizi ya kumuenzi aliyekuwa Mwenyekiti wa kwanza wa UWT, Hayati Bibi Titi Mohammed, katika Uwanja wa Ujamaa, Umwe Kusini Ikwiriri, wilayani Rufiji, mkoani Pwani jana. **PICHA: IKULU**

# Giza nene mradi stendi ya Mwenge

**Na Mwandishi Wetu**

GIZA nene limeendelea kutawala kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa kituo kipya cha daladala Mwenge uliosimamishwa Juni 20, mwaka huu.

Wakati bado taarifa ya timu ya uchunguzi wa mradi wa huo haijatoka, viongozi mbalimbali waliotafutwa na Nipashe Jumapili kuzungumzia suala hilo kuanzia ngazi ya wilaya hadi taifa, hawajatoa ushirikiano.

Timu ya uchunguzi ilipewa wiki mbili kuanzia Juni 20, mwaka huu kukamilisha kazi hiyo na kumkabidhi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu.

Timu hiyo ilipaswa kukamilisha kazi yake Julai 4, mwaka huu, lakini leo hii inatimu miezi mitatu kamili hakuna taarifa yoyote iliyotolewa na ujenzi umesimama kwa miezi minne sasa.

Nipashe ilimfuata Waziri Ummy akiwa mjini Bagamoyo Julai 18, mwaka huu kusaka mustakabali wa mradi huo, akijibu kuwa anakwenda Dodoma na kwamba Juni 19, mwaka huu alitarajia kupata mrejesho wa kamati na kuahidi kutoa majibu ya maswali atakapofika huko makao makuu ya nchi.

Tangu wiki iliyopita, Nipashe Jumapili imekuwa ikiwafuata viongozi mbalimbali wa Wilaya ya Kinondoni na Mkoa wa Dar es Salaam wakiwamo, Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe na Mkuu wa Mkoa, Amos Makalla, ambao kwa nyakati tofauti walisita kuzungumzia suala hilo, wakiomba wapewe muda zaidi.

Nipashe ilimpigia simu Waziri Ummy jana mchana bila mafanikio na hata ilipomtumia ujumbe mfupi wa maandishi (SMS) kujua kinachoendelea kuhusu mradi huo, hakujibu chochote.

Juni 20, mwaka huu, Waziri Ummy alizuru kwenye mradi huo na kueleza kutoridhishwa na kusuasua kwake na kuweka wazi kwamba amekuwa akipokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi.

"Huu mradi ulipaswa kukamilika Mei 2, mwaka huu lakini hadi sasa ni Juni na ujenzi wake umefikia asilimia 46, nasimamisha ujenzi wake kuanzia sasa na kuunda timu ya kuchunguza," alisema Ummy siku hiyo.

Waziri huyo alimwagiza Katibu Mkuu TAMISEMI kuunda timu hiyo haraka na kuitaka ifanye kazi katika kipindi cha wiki mbili, ikichunguza pia miradi miwili ambayo ni ya ujenzi wa Uwanja wa Mpira wa Manispaa ya Kinondoni na ujenzi wa jengo la utawala la Manispaa ya Kinondoni.

Mbali na hilo, Waziri Ummy pia alitangaza kumsimamisha kazi Mhandisi wa Manispaa ya Kinondoni, Isaak Mpaki, kutokana na kushindwa kuishauri vizuri Manispaa ya Kinondoni juu ya ujenzi wa miradi hiyo mitatu.

"Kuna figisu kwenye hii miradi, miradi haikamiliki, kila mtu anasema la kwake, huu mradi (stendi ya daladala) ungekamilika ungeingiza faida ya Sh. milioni 480 kwa mwaka, tungejenga shule, hospitali, lakini hadi sasa hakuna kitu," alisema.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, Spora Liana, alisema siku hiyo kuwa gharama ya ujenzi wa mradi huo ni Sh. bilioni 4.898 na kwamba mkandarasi (361 JWT Lugalo) alikabidhiwa mradi Julai 27 mwaka jana.

Alisema ilipofika Mei 2, mwaka huu ujenzi wa mradi huo ulifikia asilimia 46, hadi siku hiyo Sh. bilioni 1.558 zilikuwa zimeshatumika.

"Changamoto kubwa ni vifaa kutoagizwa kwa wakati, vibarua wachache, ambapo mkandarasi badala ya kutumia askari anaajiri raia, pamoja na kuchelewa kulipwa mishahara yao na kuja ofisi kwangu kunilalamikia," alisema Liana.

Mkandarasi wa mradi huo, Luteni Kanali David Luoga, alisema Aprili, mwaka jana walianza kazi ya ujenzi wa stendi hiyo na kazi yao ni kujenga lakini vifaa vya ujenzi vinaletwa na Manispaa ya Kinondoni.

"Ilipofika Julai mwaka jana, mtiririko wa vifaa haukuwa mzuri, vikawa vinakuja kwa kusuasua, ilipofika Septemba tuliandika barua ya kuomba vifaa vyote vinavyohitaji kufika eneo la mradi lakini hadi sasa havijafika," alisema Luteni Kanali Luoga.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**

**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA.1/2020**

**(Asilia shauri la jinai Na.82/2018, Mahakama ya Wilaya Mtwara)**

**MKURUGENZI WA MASHITAKA..........MRUFANI**

**DHIDI YA**

**HAMISI MOHAMED @NAUDENDE.............. MJIBU RUFANI**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA:HAMISI MOHAMED@NAUDENDE**
**NAMNYAMBA**
**MTWARA**

HII NI KUKUTAARIFU KUWA UNAAMRIWA KUFIKA MBELE YA MAHAKAMA KUU MTWARA KUSIKILIZA RUFAA HII MNAMO TAREHE 17/11/2021 SAA 2:30 BILA KUKOSA.

KUMBUKA KUWA ENDAPO HUTAFIKA WEWE MWENYEWE AU MTU YEYOTE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUKUWAKILISHA BASI RUFAA HII ITASIKILIZWA NA KUAMRIWA BILA WEWE KUWEPO.

IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KWA MUHURI WA MAHAKAMA LEO HII TAREHE 06/10/2021

116522802

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**RAMADHANI MZEE HANAFI** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 966 CSJ – TOYOTA CARINA** iliyosajiliwa kwa jina la **MEHBOB MUSTAFA JAPHA.** Chassis namba **AT2120043662.** Engine namba **5AH077111.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Control **No. 9910830328265.**

116528402

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**HATI YA KIAPO**

**MIMI RODGERS DOMINICK MHANDO** wa S.L.P 178 Tanga nikiwa mtu mzima na akili zangu timamu naapa na kuthibitisha mbele Hakimu Mahakamani kama ifuatavyo:

1. KWAMBA, mimi **RODGERS DOMINICK MHANDO** ni mkazi wa Donge, Tanga.
2. KWAMBA, nimepoteza kadi ya gari namba **T 708 AHL,** Nissan safari na **T 629 BSM,** Nissan Serena yenye jina la **JOHN ALMASY MOHAMED** kwamba hati zake zimeungua katika ajali ya moto Donge.
3. KWAMBA, kwa kiapo hiki naomba ofisi za TRA Tanga wanipatie kadi nyingine ya gari namba **T 708 AHL** na **T 629 BSM.**

**UTHIBITISHO**

**Mimi RODGERS DOMINICK MHANDO,** nathibitisha kuwa yote niliyoyasema hapo juu kuanzia aya 1-3 ni kweli tupu kwa jinsi nijuavyo na kwa mujibu wa sharia ya viapo (The Oaths and Statutory Declaration **Act. Cap. 34 R; E 2002).**

Imethibitishwa hapa Tanga
RODGERS DOMINICK MHANDO
Leo tarehe 22/10/2021
Mbele ya
Cheo

Sahihi ya Muapaji

116529002

## HABARI KITAIFA

## Spika Ndugai aonya wabunge kuitwa mazuzu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameoneshwa kukerwa na tabia ya baadhi ya watu kuwaita wabunge 'mazuzu', akisisitiza wana akili na ni vyema kujenga utamaduni wa kuheshimiana.

Vilevile, amezitaka Asasi za Kiraia (AZAKI) kuwa wazalendo, waadilifu kwa nchi yao na wasikubali kutumika.

Ndugai aliyasema hayo jana alipofungua maonesho ya Wiki ya AZAKI yanayofanyika jijini hapa.

Alisema lazima kujenga jamii yenye kuheshimiana, utamaduni na nia njema bila kumuonea mtu.

"Sio unaoitwa AZAKI, basi unawasema wenzako maneno unayotaka ya ovyo, tumewahi kugombana na baadhi ya wazee, mzee unatuita jina sisi hatulipendi, tumekosa nini katika kufanya hivyo?

"Hivi tumekosea wapi kama unamwita mtu jina la Juma, anasema mimi hilo jina sitaki, tatizo lako nini? Unang'anga'ania kuita hilo jina, we nani?

"Haiwezekani kama mwanadamu akikwambia hiki sina raha nacho kiache kama kweli wewe ni muungwana mtu wa Mungu.

"Matokeo yake wanakaa wazee hao wanasema wabunge mazuzu aaah, tuna akili sana, sisi hatuna muda wa kubishanabishana tu, nani anakwambia sisi mazuzu?

"Mimi kwangu watu 400,000 wananichagua kwa miaka 25 na mara mbili nimepita bila kupingwa na hata kesho nikienda kusimama tafuta wa kusimama na mimi, hutampata, akisimama mpambe wa kusindikiza, halafu wewe unaniita zuzu, yaani wale watu unamaanisha ni mazuzu wamechagua zuzu mwenzao?

"Tuheshimu watu, kwani ukimheshimu mtu tatizo lako nini? Wewe sema hoja yako itaeleweka tu na kusikika," alisema.

Kiongozi huyo wa Bunge pia alizitaka AZAKI kuepuka kubeba ajenda za watu walio nje ya mipaka ya Tanzania.

"AZAKI zinafanya kazi nzuri sana lakini wachache wenu kama hamjawahi kuambiwa na mtu mimi niwaambie wanatumika, wana ajenda zisizokuwa za kwao, wana ajenda za kupatia hela kutoka mahali fulani.

"Sasa kama we njaa yako ni hela ndio maana lazima zitungwe sheria sasa zinazokufuata kwenye hela, eeeh utatuambia nani amekupa, kiasi gani, ziko wapi, utazitumiaje na utaleta taarifa kwa kila shilingi. Zamani haikuwa hivyo, tuliaminiana, lakini baada ya kuona mwenendo...," alionya.

Alizitaka asasi hizo kuwadhibiti watu wenye tabia zisizovumilika na wasikubali kutumika huku akiwahakikishia kuwa uongozi wa nchi unawapenda wanaazaki kutokana na mchango walio nao kwenye maendeleo ya Watanzania.

Alisema Bunge lipo tayari kama asasi hizo zitataka kutoa elimu kwa mambo mbalimbali ambayo wangependa wabunge wapate.

Awali, Rais wa Foundation for Civil Society (FCS), Dk. Stigmata Tenga, alisema asasi hazishiriki kikamilifu katika mabadiliko ya sera na sheria nchini.

Alimwomba Spika Ndugai kuwasaidia kufanyike marekebisho ya sheria ya mashirika yasiyo ya serikali kuleta mabadiliko chanya kwa maslahi mapana ya taifa.



Rais wa Jamhuri ya Burundi, Evariste Ndayishimiye (kushoto) na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Geoffrey Mwambe (kulia), wakifungua pazia kuweka jiwe la msingi la kiwanda cha mbolea cha Itracom, eneo la Nala nje kidogo ya Jiji la Dodoma juzi. Kiwanda hicho ambacho mwekezaji wake ni Raia wa Burundi, ujenzi wake utagharimu dola za Kimarekani milioni 180 sawa na Sh. bilioni 415. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Shangwe mgawo mabilioni ya IMF sekta ya elimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, ameweka wazi namna zitakavyotumika Sh. bilioni 368.9 za sekta ya elimu kati ya Sh. trilioni 1.3 zilizotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Kati ya fedha hizo, wizara hiyo imepata Sh. bilioni 64.9 ambazo zitaelekezwa kwenye maeneo makuu matatu huku akibainisha kuwa wanafunzi wenye Uhitaji maalum vyuo vikuu watanunuliwa bajaj, vishikwambi na vifaa saidizi vingine.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu mpango na matumizi ya fedha hizo, Prof. Ndalichako alisema: "Kati ya Sh. bilioni 368.9 kama alivyosema Waziri wa Tamisemi, Sh. bilioni 304 zimepelekwa kwenye mambo mbalimbali ikiwamo kujenga madarasa 15,000 ambapo kati ya hayo, madarasa 12,000 ni kwa ajili ya kupokea wanafunzi ambao watajiunga na kidato cha kwanza mwaka 2022, madarasa 3,000 ni kwa ajili ya kuondoa kadhia ya shule shikizi ambazo zilianzishwa kiholela."

Alifafanua eneo la kwanza ni kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wenye uhitaji maalum ambapo Sh. bilioni 1.47 zitatumika.

"Serikali imepanga kuchapisha vitabu kwa ajili ya wanafunzi 353 wasioona na wenye uoni hafifu 3,591 wa elimu ya sekondari ambapo Sh. milioni 707 zimetengwa ili kuwa na uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja kwa elimu ya sekondari," alisema.

Alibainisha vitabu vitakavyochapishwa vitajumuisha nakala 93,366 za vitabu vya ziada vya maandishi yaliyokuzwa kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu na nakala za vitabu vya nukta nundu 9,178 kwa ajili ya wasioona kwenye shule za sekondari.

"Pia serikali itawezesha ununuzi wa vifaa saidizi kwa wanafunzi 410 wenye uhitaji maalum walioko katika vyuo vikuu 11 vya serikali ambapo Sh. milioni 770 zimetengwa," alisema.

Waziri huyo alisema vifaa vitakavyonunuliwa kwa ajili ya wanafunzi hao ni bajaj, vishikwambi, kompyuta mpakato na vifaa vingine wezeshi kulingana na mazingira yao.

Alitaja eneo jingine la pili ni kuimarisha elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ambapo kiasi Sh. bilioni 57.9 zitatumika ikiwamo kukamilisha ujenzi na kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwenye vyuo 25 vya ufundi stadi wilaya Sh. bilioni 28.76.

Alisema ukamilishaji wa vyuo utawezesha ongezeko la takriban wanafunzi 30,000.

"Serikali imepanga kukamilisha ujenzi na kuweka samani kwenye vyuo vinne vya VETA vya ngazi za mikoa Njombe, Rukwa, Simiyu na Geita Sh. bilioni 18.7 zimetengwa, vitaongeza nafasi za wanafunzi 5,600," alisema.

Pia alisema Sh. bilioni 1.04 zitajenga mabweni katika Chuo cha Ualimu wa Ufundi Morogoro, Sh. bilioni 6.8 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na mitambo ya kujifunzia vyuo 34 vya maendeleo ya wananchi na wanachuo 9,804 watanufaika.

"Katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa vitendo Chuo cha Ufundi Arusha kitapata Sh. bilioni 2.6 kwa ajili ya kujenga jengo la kitaaluma lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 911 na walimu 81," alisema.

Prof.Ndalichako alisema eneo la tatu linahusisha Sh. bilioni 5.44 zilizotengwa kuimarisha mazingira ya utoaji elimu ya ualimu kwa kujenga madarasa 41, kumbi tatu za mihadhara na mabweni 15.

Waziri huyo aliagiza watendaji wa wizara na taasisi kukamilisha miradi hiyo Mei 30, mwakani, ununuzi wa vifaa vyote uzingatie bei ya soko na matokeo ya utekelezaji wa miradi yaendane na thamani ya fedha zilizotolewa.

"Katibu Mkuu aandae mfumo wa uratibu, usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ili kubaini changamoto na kuchukua hatua stahiki kwa wakati, na kila mwezi taarifa za utekelezaji zitolewe," aliagiza.

Alionya kuwa fedha hizo sio za kulipana posho ya aina yoyote huku akisisitiza atachukua hatua kwa watakaoongeza bei ya bidhaa zisizoendana na bei ya soko kwenye miradi hiyo.


SHREE SANATAN DHARMA SABHA

24th October, 2021

NOTICE OF EXTRA ORDINARY GENERAL MEETING

An Extra Ordinary General meeting shall be held on 31st October 2021 at Shree Patel Samaj, Patel Brotherhood at 10:00am. All members of Hindu Community are invited to attend on time.

DATE : Sunday 31 October 2021
TIME : 10am
VENUE : Shree Patel Samaj Hall
AGENDA : Referendum on the proposed draft Constitution

The meeting shall seek approval and adoption of the proposed draft of new constitution of Shree Sanatan Dharma Sabha.

Yash Desai
Hon. General Secretary
Shree Sanatan Dharma Sabha

216529201

Providing Unity and Religious Leadership to the Hindu Community of Tanzania

Shree Sanatan Dharma Sabha, Pramukh Swami Street, P. O. Box 5, Dar es Salaam, Tanzania
Telephone: +255 22 2132835 Mobile: +255
Society Registration No: 463 TIN: 101-321-207
E-mail: mandir@ssds.or.tz
Web page: www.ssds.or.tz

A member of The Hindu Council of Tanzania

RIPOTI MAALUM -2

# Zebaki ilivyobeba sumu kuanzia ujauzito, mtoto hadi mazingira

## ■Inaposambaa inafika kila kona
## ■Inadhuru ngozi, figo na macho

Na Mwandishi Wetu

**SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii ilianisha picha kamili ya biashara ya zebaki na namna inavyomwathiri mtu mmoja mmoja kwa nafasi yake anavyohusika nayo. Toleo hili linaangazia mustakabali mpana kwenye afya ya mtu, kuanzia ujauzito, mtoto mchanga hadi mazingira, pia miongozo ya kisera na kisheria ikiakisi madhara hayo. Fuatilia kwa hatua...**

### WATOTO WAATHIRIKA

OFISI ya Makamu wa Rais (Mazingira) inakadiria kuwapo watoto 10,000 wanaojihusisha na uchimbaji na uchenjuaji dhahabu nchini.

Mratibu wa Mradi wa EHPMP wa Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Benjamin Mchwampaka, anafafanua madhara ya zebaki huingia mwilini kupitia vyakula kama samaki na kuvuta mvuke wa zebaki, hasa pale inapochomwa na kwenye ngozi.

"Zebaki ikiingia kwenye ngozi husababisha ugonjwa wa minamata ambao huathiri mfumo wa neva na kusababisha magonjwa kama miguu na mikono kufa ngazi na kukosa nguvu, misuli kulegea, figo kuathirika, uoni hafifu, kupoteza uwezo wa kusikia na kuongea," anasema.

Pia anataja athari zake kwenye ujauzito ama kuharibika au mtoto kuzaliwa na athari za akili, viungo pungufu, kupoteza kumbukumbu, kukosa usingizi muda mrefu, maumivu ya kichwa, kiharusi na hata kifo.

### HISTORIA YA MINAMATA

Mchwampaka anasema Minamata ni kitongoji katika Kisiwa cha Kyushu kilichoko kusini mwa Japan, ambako Aprili 21, 1956 kiligunduliwa maradhi hayo, pale msichana wa miaka mitano alipoonesha dalili za miguu kulegea na kushindwa kutembea, mwili mzima kulegea na dalili za degedege.

Wataalamu walipotafiti kiashiria hicho cha hatari kiafya, walibaini kuwapo kiwanda kinachotengeneza dawa, kikitiririsha kemikali ya zebaki kwenye mfereji wa maji machafu kuelekea baharini ilikoathiri viumbe wengi.

"Hadi kufikia Machi 2001, jumla ya Wajapani 2,265 wa kitongoji hicho walikuwa wameugua ugonjwa wa minamata na 1,784 walithibitika kufariki dunia," inafafanua ripoti ya mkasa huo.

Mtaalamu wa Mazingira wa Tume ya Madini, Abel Madaha, anasema zebaki inachafua mazingira kupitia hewa, udongo, vyanzo vya maji na inaleta athari kubwa kiuchumi kwa kuwa samaki hawatonunuliwa, pia mazao kama mboga.

Anasema mkusanyiko wa zebaki ardhini hubadilika kuwa sumu inayofyonzwa na mimea kwa mfumo wa chakula. Katika vyanzo vya maji hususani kwenye tope au mchanga, hubadilika kuwa sumu inayoliwa na baadhi ya viumbe waishio majini kama samaki.

### SERA NA SHERIA

Mtaalamu wa Mazingira, anasema Sera ya Taifa ya Madini ya Mwaka 2009, inalenga kutambua, kusaidia na kuhamasisha uchimbaji endelevu wa madini, ili kuongeza tija na mchango wa wachimbaji wadogo katika uchumi.

Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997 inatambua athari za kimazingira na kiafya zinazotokana na matumizi ya zebaki katika uchimbaji mdogo na kusisitiza usimamizi makini.

Kadhalika, Sera ya Taifa ya Afya 2007 inalenga kuboresha ustawi wa Watanzania kwa kuwanusuru walio hatarini, wakiwamo wachimbaji wadogo.

Pia, Sheria ya Udhibiti na Usimamizi wa Kemikali za Viwandani na Majumbani ya Mwaka 2003, inaelekeza udhibiti na usimamizi wa kemikali, ikiwamo zebaki.

Kuna angalizo la Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 linaloelekeza kufanyika tathimini ya athari kwa mazingira kwa wawekezaji na wachimbaji madini, wakiwamo wachimbaji wadogo kwenye dhahabu.

Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na marejeo yake miaka 2017 na 2019, inaweka utaratibu wa umilikishwaji wa maeneo kwa wachimbaji wadogo, utoaji leseni na kuzingatia usalama katika shughuli zao.

### KUTOKA BUNGENI

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Eric Shigongo, anasema uingizaji holela na utumiaji wa zebaki nchini umekuwa ukiwaathiri wachimbaji kiafya kwa kiasi kikubwa.

Anasema madhara ya matumizi ya kemikali hiyo yanatokana na wachimbaji wengi kuitumia bila ya kuwa nyenzo za kujikinga.

Shigongo pia anasema maji yanayotumika kusafishia dhahabu yakiwa yamechanganyika na zebaki, yanatiririka kwenye vyanzo vya maji kama vile mito na maziwa.

"Watu wanapotumia maji kutoka vyanzo hivyo vilivyochafuliwa na zebaki ya kuoshea dhahabu, huathirika kiafya na wakati mwingine kupata maradhi sugu yanayogharimu maisha yao," anahadharisha.

Kwa kutambua madhara hayo, Shigongo anasema kamati yao inashauri Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) ishirikiane na Ofisi ya Mkemia Mkuu kudhibiti uingizwaji na zebaki nchini.

Kiongozi huyo wa kamati pia anasema serikali inapaswa kutafuta teknolojia mbadala ambayo wachimbaji hao wataitumia ili kuachana na matumizi ya zebaki.



Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, wakiangalia shughuli za ukamataji dhahabu kwa kutumia zebaki kwenye mgodi mdogo wa dhahabu wa Mwime, Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga Oktoba 16, mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

### KINACHOFANYIKA SERIKALINI

Mtaalamu wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Maganya anataja mkakati wa kutekeleza mipango iliyopo ni kuondosha matumizi holela ya zebaki kwa wachimbaji wadogo kwa kukuza uelewa sahihi kwao kupitia mafunzo ya mbinu bora za udhibiti wa zebaki wakati wa kuchenjua.

Lingine analitaja kuwa kuwezesha upatikanaji wa fedha na utaalamu kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu, ili wahamasike na mbinu bora za kutumia zebaki, tekonolojia za uchenjuaji zisizoiweka kando zebaki.

Mkakati mwingine anaoutaja, unaenda mbali kwa kutathimini matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo, pia kukusanya takwimu zote muhimu zinazowahusu wao na nyendo zao kwa manufaa ya sekta za afya, mazingira, madini na ajira zikiwa na kanzidata maalum.

Pia wachimbaji wadogo wa dhahabu wanahusishwa moja kwa moja kudhibiti uchafuzi wa mazingira utokanao na zebaki kwenye hewa, ardhi na majini kwa kushirikisha wadau wote muhimu.

Maganya anasema ni mkakati unaoenda mbali kwa kuyaangalia makundi yote jirani na watumiaji hao wa zebaki kama vile watoto na wanawake walio katika umri wa uzazi. Katika kutekeleza hayo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Seleman Jafo, anasema kuwa wakati serikali ikiendelea na utafiti wa kutumia njia mbadala ya kuchenjua dhahabu na kuondokana na matumizi ya zebaki, wachimbaji wavae vifaa kinga wakati wa matumizi hayo ya zebaki ili kutoathiri afya zao.

Anabainisha kuwa Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI) inaonesha takwimu kubwa ya wagonjwa wenye saratani wanatoka Kanda ya Ziwa, akinyoshea kidole matumizi ya zebaki kwenye uchimbaji wa madini kuwa sehemu ya mzizi wa maradhi hayo.

Jafo anawaagiza wataalamu wa mazingira kuzuru kwenye migodi midogo ya dhahabu nchini na kutoa elimu kwa wachimbaji hao namna ya utunzaji wa mazingira pamoja na kuchukua tahadhari ya matumizi ya zebaki.

HABARI KITAIFA

# Ndumbaro azindua miradi mitano TAWA

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, amezindua miradi mitano ya maendeleo inayosimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) katika Pori la Akiba Swagaswaga wilayani Chemba na Kondoa mkoani Dodoma.

Katika uzinduzi huo juzi, waziri huyo aliongozana na Mwenyekiti wa Bodi ya TAWA, wajumbe wa bodi hiyo na Kaimu Kamishna wa Uhifadhi, Mabula Misungwi.

Miradi aliyozindua hiyo ni pamoja na: jengo la ofisi za wahifadhi wa wanyamapori; hosteli ya mapumziko kwa wageni na watalii; nyumba za kuishi za wahifadhi; na kisima cha maji chenye urefu wa mita 100 kwenda chini kinachotumia pampu za kisasa.

Alisema miradi hiyo sio tu kwamba itachochea utalii katika pori hilo, bali pia itasaidia jamii za pembezoni mwa hifadhi hasa katika upatikanaji wa maji.

Dk. Ndumbaro aliipongeza TAWA kwa kazi nzuri inayosimamiwa na Menejimenti na Bodi ya Wakurugenzi ambayo inafikia ukomo wake kesho.

# Adaiwa kuchinja wanawe na kujiua

**Na Thobias Mwanakatwe**

NG'WASHI Makigo (35) anadaiwa kuwaua watoto wake wawili kwa kuwachinja kwa kisu na kisha yeye mwenyewe kujiua.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, Blasius Chatanda, tukio hilo lilitokea Oktoba 22, mwaka huu saa 2:30 asubuhi katika Kitongoji cha Mwatambuka, Kata ya Lalago wilayani Maswa mkoani Simiyu.

Alisema siku ya tukio, watoto wadogo ambao ni Nseya Kisena (7) na Majaba Kisena (1.5) walikutwa ndani ya nyumba ya Luja Makigo wakiwa wameuawa kwa kuchinjwa.

Kamanda Chatanda alisema uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa mwanamke huyo ambaye alikuwa mkulima katika Kijiji cha Gula ndiye aliyetekeleza tukio la mauaji kwake na kwa watoto wake kutokana na kuwa na matatizo ya akili.

Alifafanua kuwa uchunguzi ulionyesha alianza kumchinja mtoto wake mkubwa wa kike (Nseya) na kisha kumchinja mtoto wake mdogo wa kiume (Majaba) na hatimaye kujichinja yeye mwenyewe.

Alisema miili ya marehemu hao imekutwa yote ndani ya chumba kimoja nyumbani kwa Luja Makigo huku kisu kinachosadikika kutumika katika kutekeleza mauaji hayo kikiwa kimebaki shingoni kwenye mwili wa mama huyo.

Kamanda Chatanda aliwataka wananchi kuongeza umakini dhidi ya watu wanaosumbuliwa na matatizo ya akili ili wasilete madhara katika jamii.

# Usalama wa wanafunzi barabarani kuimarishwa

**Na Mary Geofrey**

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la Amend, wamezindua mradi maalum wa alama za usalama barabarani utakaosaidia wanafunzi kuvuka kwa usalama.

Meneja Mkuu wa shirika hilo, Simon Kalolo, akizungumza katika uzinduzi huo juzi mkoani Dar es Salaam, alisema mradi huo utahusisha shule sita za Halmashauri ya Temeke.

Alisema alama hizo za barabarani ni pamoja na vivuko katika maeneo ya shule hizo pamoja na kutoa elimu kwa jamii, wanafunzi na walimu.

"Kitakwimu zinaonyesha kila mwaka dunia inapoteza watu zaidi ya milioni 1.35 kutokana na ajali za barabarani na wengine milioni 50 wanajeruhiwa," alisema Kalolo.

Alieleza kuwa Afrika ndio inakabiliwa na hatari kubwa zaidi ya ajali za barabarani kwa wastani wa vifo vinavyosababishwa na ajali za trafiki barabarani 26.6 kwa idadi ya watu 100,000 kulinganishwa na wastani wa dunia wa 17.4.

Meneja huyo aliongeza kuwa uwezekano wa kupoteza maisha katika ajali ya trafiki barabarani Afrika ni kubwa kuliko sehemu nyingine yoyote duniani ingawa Afrika ina idadi ndogo ya magari.

Alisema shirika hilo limekuwa likitekeleza miradi hiyo ya usalama barabarani shuleni katika nchi tisa za Afrika na kwa Tanzania wanatekeleza katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Tanga.

Mrakibu wa Polisi Mkoa wa Temeke Mussa Manyama, alisema jeshi hilo kwa kushirikiana na shirika hilo la Amend, wamekuwa wakitoa elimu ya usalama barabarani kwa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari.

"Ninawashukuru wenzetu hawa kwani pamoja na kutoa elimu pia wamekuwa wakiboresha miundombinu hususani inayohusu kuweka alama za barabarani," alisema.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Madenge, Lissy Kaluvya, alilishukuru Jeshi la Polisi na Shirika la Amend kwa mradi huo na kueleza kuwa tangu alama hizo na miundombinu iwekwe, ajali zimepungua.

"Kuna mtoto aligongwa hapa akavunjwa mguu, mwingine mbavu kwa sababu hakukuwa na alama wala matuta. Lakini sasa hali imetulia watoto wanavuka kwa usalama," alisifu.

Miundombinu hiyo ambayo ni matuta na alama za vivuko vya waenda kwa miguu, ilizinduliwa rasmi na Baraza la Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo.



Spika wa Bunge, Job Ndugai (wa pili kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Taasisi ya HakiRasilimali, Rachel Chagonja (kushoto), alipotembelea katika maonyesho ya Wiki ya Asasi za Kiraia (AZAKI) 2021, jijini Dodoma jana. Wengine ni Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Liliani Badi (wa tatu kulia), Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Legal Services Facility (LSF), Lulu Ng'wanakilala (kulia). **PICHA: MARCO MADUHU**

# Serikali kuja na mkoa wa madini

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKALI inakusudia kuanzisha mkoa wa kimadini katika Wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro kutokana na wilaya hiyo kuwa na utajiri wa madini ya aina mbalimbali ikiwamo kinywe (graphite) ambayo yamekuwa na ubora duniani.

Waziri wa Madini, Dotto Biteko, aliyasema hayo jana wilayani Ulanga alipofungua Tamasha la Ulanga Iherepa lenye lengo kutangaza fursa za uwekezaji kwenye utalii na maliasili nyingine zinazopatikana katika wilaya hiyo. Alisema Wilaya ya Ulanga ina utajiri mkubwa wa madini kutokana na kuongezeka kwa shughuli za uchimbaji madini unaobadili maisha ya wananchi wa wilaya hiyo.

Alisema kuanzishwa kwa mkoa wa kimadini kutasogeza huduma kwa wachimbaji na wawekezaji kufuatia mahitaji makubwa na kulazimika kusafiri umbali wa kilometa zaidi ya 300 kufuata huduma zinazotolewa kwa sasa ofisi ya madini mkoa iliyoko mjini Morogoro.

Waziri huyo alimwelekeza Ofisa Madini Mkoa wa Morogoro kusogeza huduma ya utoaji vibali kwenye ofisi ya madini Wilaya ya Ulanga.

Alisema kwa Tanzania, graphite imekuwa ikipatikana kwenye maeneo ya Mirerani mkoani Manyara, Ruangwa mkoani Lindi na Mahenge mkoani Morogoro ambayo imekuwa na ubora duniani inayoshindana na mataifa makubwa. "Tumetoa leseni hapa kwa ajili ya uchimbaji wa graphite. Tulikuwa na majadiliano kidogo na kampuni ya TanzaGraphite, tumehitimisha majadiliano hayo, ninaamini kabla ya Novemba kuisha, tutakuwa tumeshawapatia leseni kuanza uchimbaji," alisema.

Alibainisha kuwa uchimbaji huo utaleta mtaji kwa kuwa fedha itakayowekezwa katika kampuni hiyo, itakuwa Dola za Marekani milioni 160, sawa na zaidi ya Sh. bilioni 382.

Waziri Biteko alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameelekeza kujengwa viwanda vya kuongeza thamani kwenye maeneo yenye graphite ikiwa ni pamoja na mtambo wa kuchota graphite wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 75.

Alisema mchango wa sekta ya madini umeongezeka kutoka asilimia 3.8 mwaka 2018 hadi kufikia asilimia 6.7 mwaka 2020 na asilimia 7.7 kwa mwaka 2021 na lengo la sasa ni kufika asilimia 10 mwaka 2025.

Mkuu wa Wilaya ya Ulanga, Ngolo Malenya, alisema lengo la kuanzisha tamasha hilo ni kufungua milango ya uwekezaji katika sekta mbalimbali ikiwamo utalii, madini na kilimo.

Katibu wa wanunuzi wa madini wilayani Ulanga, Daniel Mbwambo, alipongeza serikali kwa uamuzi wa kusogeza karibu huduma za madini pamoja na kuwapo kwa soko la kuuzia madini wilayani humo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maagizo ya PAC kuhusu madeni NHC yatekelezwe

**WIKI** hii, Kamati za Kudumu za Bunge zilianza vikao jijini Dodoma ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Mkutano wa Sita wa Bunge la 12 unaotarajiwa kuanza hivi karibuni.

Moja ya kamati hizo ni ile ya Hesabu za Serikali (PAC) ambayo imekuwa ikikutana na kuhoji vigogo wa mashirika ya umma na taasisi za serikali kuhusu utendaji na matumizi ya fedha pamoja na madeni yanayokabiliwa nayo.

Juzi, mathalan, PAC ilikutana na viongozi wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na kujadili malimbikizo ya madeni ambayo linazidai wizara ya taasisi za serikali. Kwa mujibu wa taarifa ya PAC, shirika hilo linazidai taasisi hizo za serikali jumla ya Sh. bilioni 26.75, hatua ambayo inalifanya lishindwe kutekeleza majukumu yake ikiwamo miradi ya serikali ambayo limepewa kama mkandarasi.

Miongoni mwa wadaiwa sugu wa NHC kwa mujibu wa PAC, ni Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inayodaiwa Sh. milioni 692, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Sh. milioni 313), Wizara ya Fedha na Mipango (Sh. milioni 61.1) na Wizara ya Kilimo Sh. milioni 59.4.

Wadaiwa wengine ni Bodi ya Korosho Tanzania (Sh. milioni nne), Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo (Sh. milioni 250.6), Baraza la Kiswahili Tanzania (Sh. milioni 4.5), Shirika la Utangazaji Tanzania (Sh. milioni 33.6), Mkurugenzi wa Vijana Wizara ya Kazi (Sh. milioni 2.9) na Wizara ya Ardhi ambayo ni wizara mama ya shirika hilo Sh. Milioni 267.6.

Bila kuuma maneno, kamati hiyo ilisema shirika hilo, kutokana na kuzidai taasisi hizo, linashindwa kutekeleza miradi yake kwa wakati ikiwamo ile ya serikali licha ya kufanya kazi kwa weledi.

Kutokana na madeni hayo, ni ukweli usiopingika kwamba shirika hilo ambalo miaka ya karibuni lilipata sifa kemkem kwa kutekeleza miradi mikubwa na kufanya mageuzi makubwa ya kiutendaji linaweza kuporomoka kama hatua za makusudi hazitachukuliwa.

Kuna msemo kwamba mjenga nchi ni mwananchi na mbomoa nchi ni mwananchi mwenyewe. Msemo huo kwa sasa unasadifu hali halisi iliyoko ndani ya NHC kwamba serikali yenyewe ambayo ilichukua jitihada za makusudi kulisuka upya shirika hilo, ndilo linalotaka kuliporomosha kutoka kule lilikokuwa miaka 10 iliyopita.


Tunasema hivyo kwa sababu madeni makubwa ambayo NHC inadai yako mikononi mwa serikali ikiwamo wizara mama ya shirika, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Madeni hayo yanaweza kukwamisha juhudi za shirika kujiendesha pamoja na utekelezaji wa miradi, ikiwamo ya ujenzi wa nyumba zake kwa ajili ya kuuza na kupangisha ili kuongeza ukwasi wake pamoja na mirdi ya serikali, ikiwamo ujenzi wa hospitali za rufani za kanda Mtwara na Chato, NHC ikiwa mkandarasi.

Serikali imekuwa ikiipa NHC miradi ya ujenzi kama iliyotajwa hapo juu lakini malipo yake yamekuwa yakisuasua hatua ambayo inakwamisha shirika kutekeleza kazi zake na kumaliza ujenzi wa miradi hiyo kwa wakati.

Kama ambavyo PAC iliagiza juu ya kulipwa kwa madeni hayo, ni wakati mwafaka sasa kwa taasisi za serikali zinazodaiwa, kuona umuhimu na kuweka mipango ya kulipa zinazodaiwa na shirika hilo ili kuliwezesha kusonga mbele katika majukumu yake na kustawi zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Ugonjwa huu usigeuzwe sababu wanandoa kukimbiana

**KICHWA** kikubwa na mgongo wazi, ni miongoni mwa magonjwa yanayotajwa kuumiza familia kutokana na baadhi ya wanaume kukimbia wenzi wao wanaojifungua watoto wakiwa na ulemavu huo.

Hali hiyo inaelezwa kuwa inaacha simanzi pale mtu anapoamua kukimbia familia au kumfukuza mke wake, huku chanzo cha kuchukua hatua hiyo kikielezwa kuwa ni uelewa mdogo kuhusu ugonjwa huo.

Wakati baadhi ya wanaume wakichukua hatua hizo, inaelezwa kuwa kuna haja ya kutoa elimu zaidi jamii ijue chanzo cha ulemavu huo, ili kunusuru ndoa zisiendelee kusambaratika, badala yake wazazi washirikiane kulea watoto wao.

Katika mkutano wa Chama cha Wazazi Wenye Watoto wa Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazazi Tanzania (ASBAHT), liliibuka suala hilo la baadhi ya wanaume kukimbia au kufukuza wake zao.

Kikao hicho kilifanyika Dar es Salaam, kujadili maandalizi ya maadhimisho ya Siku ya Watoto Wenye Vichwa Vikubwa na Mgongo Wazi, yanayotarajiwa kufikia kilele kesho Oktoba 25.

Mratibu wa ASBAHT, Hidaya Alawi, alisema chama hicho kina wanachama 2,545 lakini asilimia 70 ya ndoa za wanachama hao zimesambaratika kutokana na wanaume kukimbia wake zao au kuwafukuza.

Ajabu ni kwamba, wanaume wanakimbia familia zao, huku madaktari wakihimiza umuhimu wa kuzingatia lishe bora, hasa vyakula vyenye wingi wa madini ya foliki asidi kama mboga za majani.

Wanataja mboga hizo kuwa ni mchicha, spinachi, kabichi na vingine vingi ambavyo vipo maeneo mengi nchini, lakini pia matunda kama maembe, maparachichi, mapapai na ndizi.

Vyakula vingine ambavyo madaktari wanavitaja kwa ajili ya kuimarisha afya ni vya nafaka kama mahindi, mihogo na mazao jamii ya kunde, pia mayai, samaki, nyama na maini.

Sharti ni kwamba, wazazi wote wahakikishe wanapata lishe yenye madini ya foliki asidi ambayo yanapatikana kwenye vyakula ambavyo wamekuwa wakivitaja, iwe ni miezi miwili na nusu au mitatu kabla ya kubeba ujauzito.

Hatua nyingine ni mama kumeza kidonge cha foliki asidi kila mara kabla, wakati na baada ya ujauzito, kwa lengo hilo la kumuepusha kuzaa mtoto mwenye ulemavu huo.

Kwa elimu hiyo ni kwamba, mwanamume hana haki ya kumfukuza au kumkimbia mke wake anayejifungua mtoto mwenye ulemavu huo kutokana na kwamba kila mmoja ana sehemu yake katika uzazi.

Mbali na hayo, madaktari wanaeleza kuwa, mtoto anaweza kuzaliwa akiwa mzima mwenye afya. lakini baadaye akaja kupata ugonjwa wa kichwa kikubwa baada ya kuugua au kupata kuumia kichwa.

Katika ufafanuzi wao ni kwamba, mtoto akiumia kichwa kisha damu ikavujia kwenye ubongo au kuumwa ugonjwa wa uti wa mgongo, vinaweza kusababisha akapata ulemavu wa kichwa kikubwa.

Iwapo hali yenyewe ndiyo hiyo, wanaume wanapata wapi haki ya kufukuza au kukimbia wake zao? Ninadhani ipo haja ya kuwaelimisha ili watambue kuwa kila mmoja ana nafasi katika kumlea mtoto mwenye ulemavu huo.

Kufukuza au kumkimbia mke ninaona si njia sahihi, bali tatizo hilo likishatoa kwenye familia, ni kulikubali na kisha kukabiliana nao, hasa kumuwaisha haraka mtoto hospitali ili apate huduma zinazostahili.

Binafsi, ninaamini kuwa kwa maelezo ya madaktari, ni wazi kwamba tatizo kama hilo linaweza kumkuta kila mtu kwenye familia yake, anaweza kuzingatia masuala ya lishe, lakini likatokea baada ya mtoto kuzaliwa.

Hivyo, kwa mtazamo wangu ni kwamba, si vyema kukimbia tatizo, bali ni kulikabili tangu mwanzo hadi mwisho, kwani sidhani kuna mzazi anapenda kuzaa mtoto mwenye tatizo la kiafya.

Pamoja na hayo, ingependeza kama wazazi hawatakuwa chanzo cha kusambaratisha ndoa za watoto wao kwa sababu ya kuzaa watoto wenye ulemavu huo, badala yake wawatie moyo ili walee mtoto wao.

Ninagusia hilo, kwa sababu katika kikao cha ASBAHT inaelezwa kuwa baadhi ya wazazi wamekuwa chanzo cha kusambaratisha ndoa za vijana wao kwa kuwaambia kuwa kuzaa mtoto mwenye ulemavu huo ni mkosi.

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Tanzania tuendelee kutumia GMO?



Na Pascal Mayalla

**Prof. Mkenda alisema TOSCI imefanya kazi nzuri ya kurahisisha uhakiki wa mbegu kwa wakulima kwa kutumia njia za kisasa za kielektroniki, kuhakiki mbegu kwa kutumia simu ya mkononi, hivyo kuliwezesha taifa kutumia mbegu zenye ubora uliothibitishwa na TOSCI.**

WIKI iliyopita nilikuwa mjini Moshi kwenye maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani, yaliyofanyika katika viwanja vya Pasua. Maadhimisho hayo yaliandamana na maonyesho ya wiki nzima ya chakula.

Siku yenyewe ya chakula duniani ni Okotba 16, kila mwaka lakini ilitokea tu kama bahati, Rais Samia Suluhu Hassan alikuwa kwenye ziara ya kiserikali mkoani Kilimanjaro.

Kutokana na umuhimu wa chakula kwa binadamu, nilitaraji serikali ya mkoa ingepiga ndege wawili kwa jiwe moja, kwa Rais Samia kuja kutembelea maonyesho ya Siku ya Chakula Duniani na kuyahitimisha siku ya kilele lakini haikuwa hivyo. Kilichofanyika ni kuisogeza mbele siku hii muhimu kuli kuipisha ziara ya Rais.

Kwa maoni yangu, nikiangalia shughuli zote ambazo Rais Samia alikwenda kuzifanya mkoani Kilimanjaro, hakuna hata moja inafikia hata nusu ya umuhimu wa Siku ya Chakula. Ni lazima tukubali kutofautiana, kila mtu ana mtazamo wake wa kipi ni muhimu kuliko kingine. Lakini kwangu, kitu muhimu cha kwanza ni Mungu aliyetuumba, cha pili ni hewa tunayovuta na cha tatu ni chakula. Haya tuyaache yameishapita.

Moja ya mambo mazuri kabisa ya Siku ya Chakula Duniani ni pamoja na Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), kushinda tuzo ya banda bora.

Kutokana na ushindi huo, Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, alipongeza taasisi hiyo kwa kazi nzuri, iliyosababisha kufikia mafanikio hayo na kuwasisitiza wakulima wote wa Tanzania, kutumia mbegu zenye alama ya TOSCI ambazo ndizo mbegu zilizothibitishwa kutumika nchini.

Prof. Mkenda alisema TOSCI imefanya kazi nzuri ya kurahisisha uhakiki wa mbegu kwa wakulima kwa kutumia njia za kisasa za kielektroniki, kuhakiki mbegu kwa kutumia simu ya mkononi, hivyo kuliwezesha taifa kutumia mbegu zenye ubora uliothibitishwa na TOSCI.

Waziri pia aliisifu TOSCI kuyatumia maonyesho hayo kutoa elimu kwa umma, si tu kwa wananchi waliofika viwanjani, bali pia banda la taasisi hiyo lilitoa elimu kubwa kupitia vipindi vya redio na TV ambavyo vilioonekana kwenye TV mbalimbali.

Waziri Mkenda alisema serikali ya Awamu ya sita, chini ya Rais Samia, imepania kufanya mapinduzi ya kweli ya kilimo na kutoa umuhimu wa pekee kwa utafiti ambapo bajeti ya utafiti imeongezwa maradufu. Bajeti hiyo haijajumuisha Sh. bilioni nane zilizotolewa na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) kwa serikali ya Tanzania, kwa kuzielekeza kwenye utafiti.

Akizungumzia umuhimu wa utafiti, Prof. Mkenda alisema: "Naamini huko tunakowenda, utafiti ni suala muhimu sana kwenye kilimo kuliko ambavyo tumeweza kuamini zamani, ili kuendana na mbadiliko ya tabia nchi, kuendana na mazingira yetu, kuendana na aina ya udogo na afya ya udongo tunaotumia, lazima tufanye utafiti."

Prof. Mkenda aliendelea kwa kutoa mifano akisema: "Unapotumia mbolea, lazima ujue udogo wa hapo unahitaji nini na ili ujue udongo unahitaji nini, ni lazima tufanye utafiti, hivyo bajeti ya Wizara ya Kilimo, tumeiongeza zaidi ya mara mbili. IFAD imetupa zaidi Sh. bilioni nane ambayo pia itakwenda kwenye masuala ya mbegu".

Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI, Patrick Ngediagi, alisema ushindi huo ni faraja kubwa kwa TOSCI nzima, menejimenti na wafanyakazi wote ambao wanajituma kwa bidii, na unazidi kuwahamasisha na kuwapa ari ya kuendelea kujituma zaidi na zaidi, kuwatumikia Watanzania.

Gwediagi aliwasisitiza wakulima kote nchini kuhakikisha wanatumia mbegu bora na namna pekee ya kutambua mbegu ni bora, ni kupitia alama ya TOSCI, hakuna namna nyingine.

TOSCI imeshiriki kwa kishindo maonyesho ya Siku ya Chakula Duniani yaliyofanyika kitaifa mjini Moshi mkoani Kilimanjaro. Kishindo hicho si tu kujiongeza na kutoa elimu kwa wananchi pekee waliopita kwenye Banda Lake, bali elimu kwa Watanzania wengi zaidi kupitia mfululizo wa vipindi vya TV vya TOSCI, vilivyoonekana kwenye vituo mbalimbali vya TV.

Pamoja na Tanzania kuwa nchi inayotegemea kilimo, tuna ardhi kubwa yenye rutuba ya kutosha na vyanzo vya kutosha vya maji kufanya kilimo cha umwagiliaji, hivyo kujitosheleza kwa chakula na ziada tuuze nje.

Lakini ni jambo la ajabu sana, Tanzania bado hatujajitosheleza kwa chakula na kutufanya tuagize hata tunaagiza mchele kutoka nje! Pia tunaagiza sukari kutoka nje pamoja na mafuta ya kula hata ngano kwa sehemu kubwa. Si hivyo tu hata 'apples' zote na zabibu kwenye 'supermarket' zinatoka nje.

Swali ni je, sasa ni wakati muafaka wa Tanzania kutumia mbegu za GMO ili kuliwezesha taifa kujitosheleza kwa chakula na ziada tuuze nje?

**pascomayalla@gmail.com**
**0754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo



Na Joseph Kulangwa

**Hivyo ni jukumu au dhima ya mzazi yeyote mwenye nia njema ni kuhakikisha anafuatilia nyendo za watoto wake kila waendako na kila waliko ili kuchelea kupata sifa mbaya katika jamii.**

FAMILIA nyingi duniani, kama si zote, hufurahia kuona zinaishi na kukua katika mazingira yenye nidhamu nzuri, hususan watoto kwa sababu ndio taswira ya familia husika.

Mzazi akisikia mwanawe huko nje ana tabia mbaya, hujisikia vibaya pia. Lakini asikiapo mwanawe ana nidhamu nzuri mtaani, hujisikia fahari na kujisifu kwa uzazi wake.

Mtoto akiharibikiwa, ndivyo pia familia huharibikiwa na kupelekewa sifa hasi kwamba imeshindwa kulea watoto na sasa ni vibaka, majambazi, wauaji au malaya.

Hivyo ni jukumu au dhima ya mzazi yeyote mwenye nia njema ni kuhakikisha anafuatilia nyendo za watoto wake kila waendako na kila waliko ili kuchelea kupata sifa mbaya katika jamii.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba litokeapo baya kufanywa na mtoto au watoto, alaumiwaye daima ni baba au mama na hatimaye familia nzima huonekana haina maana katika eneo iishimo.

Viongozi katika jamii ni sawa na wazazi katika familia, hivyo wanapokuwa wameteua au kuweka watu madarakani, kuwawakilisha, huwa wameteua taswira zao katika jamii. Wawakilishi hao waharibupo, huharibu taswira ya jamii.

Hali hii huenda mpaka kufikia ngazi ya taifa kwamba viongozi wa kitaifa wanapoteua wawakilishi wao tuseme mikoani, huhakikisha kwanza wanajua tabia na nyendo zao kabla ya kuwateua.

Taifa la Tanzania limepitia katika hali hii tangu lilipopata Uhuru wake, likiitwa Tanganyika na mpaka lilipoungana na Zanzibar na kuzaliwa Tanzania.

Viongozi wake walikuwa na wamekuwa wakifanya uteuzi wa wawakilishi wao kwa kuangalia tabia na nyendo zao na sifa zingine za kiongozi. Mara zote wateuliwa huonekana kama watoto wa wateuzi kwa kuwa ndio huwawakilisha.

Itokeapo kiongozi akabananga dhamana aliyopewa kutokana na tabia yake, basi humdhalilisha aliyemteua, hivyo mteuzi hustahili lawama hasa pale anapomshuhudia mteule anabananga na kumnyamazia.

Miaka michache iliyopita, tulishuhudia wateule wakifanya mambo ambayo mtu wa kawaida anashindwa kuyasimulia. Lakini tulinyamaza kimya kwa kuhofia 'ndimi kukatwa' mpaka mahakama moja ilipoamua kutufunua macho na kutuzibua masikio kumbe kuna mteule alikuwa akifanya yake kwa kutumia dhamana aliyopewa, akitenda uovu wa kutumia silaha kujipatia kipato na kusingizia kutumwa na mkubwa aliyemteua! Watu hivi sasa wanaulizana ilikuwaje yakafanyika hayo huku akiangaliwa tu?

Si yeye peke yake, mbona walikuwapo wengine wakitenda na kutamka mambo ambayo yalitia ukakasi lakini kwa kuchelea 'ndimi kukatwa' hatukufunua midomo kutamka lakini tukishuhudia kwa macho tu na kuumia kimoyomoyo.

Nani hakupata kusikia mmoja akivamia kituo cha televisheni akiwa na mitutu na askari, eti kwenda kulazimisha kipindi kinachomchafua hasimu wake kitoke? Alipochunguzwa na kubainika kakosea, mnajua nini kiifuata?

Nani asiyejua kuwa katika mlolongo huo, Waziri alishikiwa mtutu hadharani kwa kuwa alimgusa mteule huyo mvamizi wa kituo cha habari? Hakufanywa lolote hata pale alipotaka kukwepa kodi ya makasha bandarini! Mengine ni kumwachia Muumba tu!

Akawapo mwingine aliyethubutu kuwatukana viongozi wastaafu wetu, si viongozi tu bali marais wastaafu akiwaita wazee wanaowewESEKA, akiwataka wajikalie vijijini huko eti kwa sababu enzi zao zilishapita, hivyo nao kupitwa na wakati!

Ilisikitisha kusema hivyo na kutukumbusha jinsi Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, alipokuwa ameng'atuka, alivyokuwa akiendelea kutusema na kulisema taifa pale alipogundua nyufa kwenye nyumba yetu.

Waliokuwapo miaka hiyo ya 1990 wala hawakufunua vinywa kumsema na tena walimshangilia na kumshukuru kwamba alikuwa akituonesha njia. Lakini watoto wa sasa wanawasema wastaafu kuwa watulie ya kwao walishayamaliza! Alinyamaziwa tu na bado yupo!

Wengine kama huyo wakaibuka kutoa kauli za kutaka wapinzani wauawe, vibaka wauawe, wakosaji wauawe! Kifupi sheria zichukuliwe mikononi tu kana kwamba nchi haina ustaarabu, haina sheria, haina Katiba! Nao wakanyamaziwa tu na utawala. Hadi Mungu alipotuletea Chifu Hangaya, naye akasema inatosha.

Lakini bado wamo katika serikali, tumwombee tu Chifu Hangaya akae sawa atuondolee mbali na wachunguzwe kwa maumivu waliyoyasababisha kwa Watanzania wenzao ili haki si tu itendeke, bali ionekane imetendeka. Au siyo?

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Waziri Makamba wamulike REA Mbulu



Na Thobias Mwanakatwe

KATIKA maisha yangu namshukru Mungu nimefanikiwa kutembelea mikoa na wilaya zote za Tanzania Bara. Waswahili wanasema unapotembea sana maeneo mbalimbali iwe ndani au nje ya nchi, unajifunza mambo mengi na kuziona changamoto wanazokumbana nazo wananchi.

Baada ya wiki iliyopita kuitembelea Wilaya ya Karatu mkoani Arusha hususani mjini Karatu, safari hii nikaona ni vyema nifike katika Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, hizi ni wilaya jirani.

Umbali wa kutoka Karatu mjini kwenda Mbulu mjini ni takribani kilometa 74. Barabara yote ni ya vumbi na usafiri mkubwa na magari ya abiria ni Toyota Land Cruizer ambazo zinatumia saa moja na nusu kutoka Karatu hadi Mbulu mjini. Mbulu ni moja ya wilaya katika Mkoa wa Manyara na kwa mujibu wa Sensa ya Watu na makazi ya mwaka 2012, inakadiriwa kuwa na wakazi 320,279 waishio humo.

Mbulu imepakana na Mkoa wa Arusha pamoja na Ziwa Eyasi upande wa kaskazini, Wilaya ya Babati upande wa mashariki,

Wilaya ya Hanang upande wa kusini na Mkoa wa Singida kwa magharibi. Wenyeji asilia ni hasa Wairaqw (Wambulu). Mwaka 2015 wilaya iligawanywa katika majimbo mawili ya Mbulu Mjini na Mbulu Vijijini. Kwa wasiojua historia ya nchi hii, Mbulu ni moja ya Wilaya kongwe nchini.

Baada ya kufika Mbulu mjini ili kufika msibani, mwenyeji wangu aliniambia nipande pikipiki na nikampata dereva wa bodaboda aitwaye Tinu, akanipeleka hadi katika kijiji cha Landa Mbulu Vijijini.

Nikiwa njiani, nilishuhudia Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) wamejitahidi kuchonga barabara ingawa maeneo mengine hususani katika kitongoji cha Tlawi, uchongaji wao umenipa shaka kwani unahatarisha maisha ya watumiaji.

Ni kwamba katika kitongoji hicho, barabara imechongwa lakini yameachwa magema mithili ya handaki ambayo nina hakika mvua zikianza kunyesha, yatabomoka na kuziba barabara. Hii ni hatari kwani mtu anaweza akasema ajifiche kukwepa mvua kutokana na jinsi magema hayo yalivyo.

Sina mpango kuzungumzia suala la barabara bali nataka nijikite zaidi kuzungumzia mradi wa usambazaji umeme vijijini chini ya Wakala wa Umeme Vijiji (REA) katika Wilaya ya Mbulu hasa maeneo ya vijijini.

Serikali ilianzisha miradi hiyo kwa lengo zuri la kuhakikisha wananchi wa vijijini nao wanapata huduma ya umeme ili angalau wafanane na wenzao wa mijini ambao huduma hiyo ilifikia siku nyingi.

Pamoja na nia hiyo nzuri ya serikali, bado kuna baadhi ya wilaya watendaji wa REA hawawatendei haki wananchi wa vijijini kutokana na kuwanyima huduma hiyo muhimu bila sababu zozote za msingi. Mfano ni katika wilaya ya Mbulu. Ukitokea Mbulu mjini ukapitia vijijini vya Anslay, Landa na Banee, utaona REA walivyojitahidi kusimamisha nguzo za umeme na nyaya ziko tayari lakini vitongoji katika vijiji hivyo vimeachwa bila kufikishiwa umeme. Badala yake umeme umeenda moja kwa moja hadi Kijiji cha Banee.

Maeneo mengi ya vitongoji vya Kijiji cha Landa vyenye nyumba za wakazi yakiwamo makanisa, hawajapewa huduma ya umeme, wamebaki kushangaa nguzo zikiwapita. Mfano wa vitongoji vilivyokosa huduma hiyo ni katika Kijiji cha Landa. Ukizungumza na wenyeji wanakwambia wameshaomba mara kadhaa kwa watendaji wa REA wawawekee huduma hiyo lakini wanapigwa porojo tu.

Mchungaji wa kanisa moja akasema amejitahidi hadi kuwasiliana na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wamsaidie kanisa lake lipate umeme lakini jitihada hizo bado hazijazaa matunda kutokana na ukiritimba ulioko ndani ya REA. Nikizungumza na wananchi wa vitongoji cha Tawli na Dimay vilivyoko katika kijiji cha Landa, wanasema wamewasilisha maombi ya kupatiwa umeme mara kadhaa lakini viongozi na watendaji wa REA wamezima masikio. Kanisa hawataki kuelewa.

Hapa ndipo ninaposema Waziri wa Nishati, January Makamba, ajaribu kuwamulika watendaji wa REA katika wilaya ya Mbulu.

Nadhani watendaji hawa hawana nia njema kwa wananchi na bila shaka wanataka kupunguza kura za Chama cha Mapinduzi (CCM) katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Kimsingi, malalamiko ya wananchi wa kijiji cha Landa ni mengi lakini ninavyokufahamu kwako Waziri Makamba, kilio hiki cha wananchi ambacho watendaji wa REA wamekiona kama ni kilio cha samaki, kina madhara makubwa kwa serikali katika uchaguzi ujao.

Makamba, katika jimbo lako la Bumbuli, Wilaya Lushoto, mkoani Tanga, umefanya vizuri kwani wakati unaingia madarakani, ulikuta kata nne tu ndizo zilikuwa na huduma ya umeme lakini hivi sasa kata 15 kati ya 18 katika jimbo hilo tayari zimeshafikiwa na huduma hiyo. Umeyafanya hayo ukiwa mbunge na pengine sifa yako ya kutekeleza vyema ahadi na kuwajali wananchi wako ilimshawishi Rais Samia Suluhu Hassan kukupa wizara nyeti ya Nishati akijua utaitendea haki.

Nakumbuka Agosti, mwaka huu, Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato alifika wilayani Mbulu na kuliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Manyara kuwaunganishia umeme wananchi wote waliolipia gharama zinazohitajika kabla ya mwezi huo kumalizika.

Sina hakika kama hili limetekelezwa maana kilio cha wananchi bado ni kikubwa hususan maeneo ya vijijini. Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Sezaria Makotha, alimweleza Naibu Waziri kuwa Vijiji 48 vya wilaya hiyo Kati ya 110 vimeshapata Umeme.

Kwa mantiki hiyo, utaona vijiji karibu 62 havina huduma ya umeme na hapa ndipo ninaposema TANESCO na REA Mbulu bado kuna uzembe sana. Mheshimiwa Makamba anza na hawa watakuangusha.

Lakini pia Mbunge wa Mbulu Vijijini, Flatey Massay, najua wewe ni mtaalam wa kuruka sarakasi, basi jitahidi ruka sarakasi umfikishie Makamba kilio cha wananchi wa kijiji cha Landa na maeneo mengine kukosa umeme.

**Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Wilaya ya Mbulu. Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe 2005@yahoo.com**

## DARASA LA NDOA

# KINABABA MSITELEKEZE FAMILIA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

BABA ni msingi wa familia. Uwapo wa baba katika familia ni muhimu kwa kuwa baba ni mbeba maono na mwekezaji wa misingi ya nidhamu na ustawi wa familia yake. Baba anapotimiza majukumu yake, anaweka misingi imara ya nidhamu, heshima, ustawi na maadili mema.

Maandiko Matakatifu ya Mungu yanaainisha nafasi na wajibu wa baba katika familia. Jukumu la msingi alilopewa baba ni kuitunza na kuwa kiongozi wa familia yake (most sacred responsibility). Kina baba wanategemewa kuwa na uwezo wa kuongoza na kutunza familia zao.

Nidhamu, heshima, ustawi na maadili mema hujengwa pale baba anapompenda mke wake, anaposikiliza watoto wake, anapowatunza, anapowafunza, anapowaonya, anapowarekebisha, anapowaadabisha, anapoweka kanuni na miongozo mbalimbali ya kusimamia familia ili kujenga familia imara.

Baba anapotimiza majukumu yake anaongeza na kutunza thamani, mamlaka, na nafasi yake kwa familia. Baba anayewajibika na kuwa na muda na familia yake ni uthibitisho dhahiri wa kujali na kutoa kipaumbele kwa wale wa nyumbani mwake.

Tunaanza kuzoea kusikia kwamba jamii yetu ya leo ni jamii isiyokuwa na kinababa.

Nafasi na maana ya baba inaanza kukosekana na kupotea. Hii ni kwa sababu baadhi ya akina baba kwa kisingizio cha kazi, majukumu na mambo mengine binafsi, wamejitenga na kutelekeza familia zao. Mamlaka ya kinababa wengi katika jamii ya leo, yameanza kutiliwa shaka. Ziko baadhi ya familia ambazo baba awepo au asiwepo mke na watoto hawaoni tofauti yoyote. Awepo sawa, asiwepo sawa. Hali hii ni hatari kubwa kwa mustakabali wa familia.

Wako baadhi ya kinababa ambao hawawajibiki katika familia zao (irresponsible fathers). Wamebaki na sifa ya kuwa mwanamume mashine na kupoteza sifa na maana halisi ya kuwa baba. Kimsingi, kinachomfanya mwanamume aitwe baba, si maumbile yake bali majukumu aliyoyabeba kwa ajili ya familia yake. Hivyo, baba asiyewajibika na anayetelekeza familia yake ni muuaji na anapoteza sifa ya kuitwa baba. Mwenyezi Mungu amemweka baba katika familia ili kupitia heshima, hadhi na utambulisho wake kama mwanamume, awajibike, kuwa karibu na watoto na mke wake na kushirikiana naye kila kitu, furaha na huzuni, matumaini na changamoto zingine. Wako kinamama wameolewa lakini maisha wanayoishi hayana tofauti na kinamama wasio na waume (single mothers). Jambo la msingi ni kwamba inafaa baba aitunze familia yake, awepo na kupatikana kwa ajili ya mke wake na makuzi ya watoto kwa kuwa baadhi ya kinababa wapo lakini hawapatikani. Baba asiyekuwa na muda na familia yake, anapoteza thamani na umuhimu wa uwapo wake. Uwapo wake unakuwa hauna mguso (impact) kwa mke wake na watoto kwa sababu hapatikani nyumbani. Waingereza wanasema "Life is measured by impact and not by being present." Kwa hiyo, si jambo zuri na ni kinyume cha Neno la Mungu mke na watoto kumkosa baba pasipo ulazima au mke na watoto kubeba majukumu ambayo kimsingi baba alipaswa kuyabeba.

Familia nyingi zimekosa kufurahia uwapo wa baba kwa sababu muda mwingi baba hapatikani nyumbani. Katika hali isiyotarajiwa, unakuta mke anapoteza hisia (feelings) na mvuto dhidi ya mume wake. Watoto nao wanapoteza upendo kwa baba yao. Wanamwona baba yao ni mtu mkatili asiye na upendo.

Hali hii imesababisha watoto wengine wakiwa watu wazima, thamani na umuhimu wanaelekeza kwa mama zaidi kuliko baba kwa sababu ndiye aliyekuwa na muda nao. Kinababa wengi wakiisha kuleta mahitaji ya nyumbani, wanaona wamemaliza. Wanasahau kwamba kutunza familia ni zaidi ya kutoa mahitaji ya nyumbani. Familia inamhitaji baba zaidi kuliko vitu au mahitaji wanayopewa. Ukaribu wa baba kwa familia yake ni muhimu sana. Baba anapokuwa na muda na familia yake, mke na watoto wanajisikia kuwa salama na kupendwa. Kwa mantiki hiyo, thamani na umuhimu wa uwapo wa baba katika familia unaongezeka.

Pamoja na majukumu mengi waliyo nayo kinababa, ni muhimu kutengeneza muda wa kuwa na familia. Ni muhimu kufanya kazi kwa ajili ya maisha lakini ni muhimu zaidi kuwa na muda wa kazi na muda wa familia (work is important, so is your family). Kwa maana hiyo, kazi isiwe kisingizio cha kudumu cha kukosa muda na familia. Baba asiyetengeneza muda wa kuwa na familia, anatengeneza bomu litakalomlipukia mwenyewe, litakalomjeruhi na kumwangamiza wakati wowote.

Kwa upande mwingine, kinamama wanao wajibu wa kutengeneza mazingira ya kuvutia nyumbani ili waume zao waone nyumbani ni mahali pa kuishi na kustarehe. Nasema hivi kwa sababu baadhi ya kinamama wamekuwa sababu ya waume zao kuwa mbali nao kutokana na dharau, ujeuri, ukorofi na meneno yao makali. Kinamama wanao wajibu wa kuhakikisha waume zao wanajisikia ni wafalme (kings) ndani ya nyumba na wao kuwa malkia wa nyumba (queens of the household).

Inapendeza na kutia moyo pale familia inapomfurahia baba na baba anapoifurahia familia. Furaha ya familia hualika uwapo wa Mungu na baraka katika familia.

Wewe baba mwenzangu, usiwe sababu ya kuleta upweke na kuondoa furaha ya familia yako. Ikumbukwe kwamba wakati wote baraka au laana kwa yale tunayohangikia, huanzia katika familia. Kwa hiyo, kazi na majukumu visiondoe utu wako na thamani ya familia yako.

**■Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

OKTOBA 24, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 14


## Namna ya kutengeneza mkate bora wa mahindi



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Dondoo jinsi ya kuchagua mitungi ya mapambo



## HARUSI

Ukurasa 12



# Maajabu ya kurejesha urembo wa kucha

Ukurasa 14

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



A. 1 3 5 7 9 11 13 15

B. 2 4 6 8 10 12 14


C. 17 19 21 23 25 27

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | S | H | A | K | A |
| ■ | U | ■ | ■ | I | ■ |
| A | K | A | ■ | B | ■ |
| ■ | A | ■ | P | A | O |
| ■ | R | ■ | ■ | L | ■ |
| P | I | M | B | I | ■ |

## AMSHA AKILI





## TOA TOFAUTI 5




## WATOTO

# PAKA RANGI




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
UPE, PUA, SIMBA, PASHA, PEPONI, HURUMA

## CHEKA



Alichokifanya daktari

MAMA John alikwenda dukani kumnunulia mwanawe viatu vya shule, aliporudi alimpatia viatu vile akiwa na furaha.

**Mama:** Mwanangu leo nimekuletea zawadi ya viatu.

**John:** Mama asante nitakwenda kuwaonyesha akina Juma.

**Mama:** Sawa lakini yule baniani kanambia kama hujakipenda nirudishe.

**John:** Mama basi huyo ni mtu mwema sana kwani mwalimu alitufundisha kuwa baniani mbaya kiatu chake dawa.

**Mama:** Haa! Huo ni msemo tu ukimaanisha kila kitu unachokidharau sasa, kinaweza kukusaidia baadaye.

**Swali**

Mto Ruvuma unapatikana katika mkoa gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Usaliti unavyoweza kuanzisha migogoro

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada yetu kuhusu vyanzo vya migogoro katika maisha yetu ya kila siku. Tayari tumeona migogoro binafsi na ile ya marafiki pamoja na itokanayo na mazingira.***

LEO tumulike usaliti, uzembe na hofu katika maisha yetu.

Chanzo kingine cha mgogoro ni usaliti. Pengine wewe uko kwenye kazi na uliahidiwa marupurupu mengi lakini mwisho wa siku hupewi na muda umepita. Hapo lazima utakosa uvumilivu.

Sasa hapo utaanza kutengeneza mgogoro na mwajiri wako kwamba hivi imekuwaje? Huyu mwajiri aliniahidi kitu fulani lakini hadi sasa mambo hayako hivyo. Lazima utajiona kwamba umesalitiwa kwa kutotimizwa ahadi uliyopewa.

Usaliti pia umejikita kwenye uhusiano. Wako watu husema pendo kati ya watu wawili ni jambo lisiloeleweka, hapana. Pendo unaweza kulivuruga wewe mwenyewe.

Kwa mfano, unaingia kwenye uhusiano na mtu, huku wewe mwenyewe hujui malengo unayoyahitaji kwenye maisha yako. Au inaweza kutokea kwamba una uhusiano na mtu ambaye hana vipaumbele vinavyofanana na vyako.

Wewe unapenda mpira, yeye anapenda Kamari. Unapenda kwenda kwenye nyumba za ibada lakini yeye anapenda kwenda kumbi za starehe. Kwa mantiki hiyo, kuna muda unapaswa kutulia ili kumfahamu vizuri mtu ambaye unaishi naye.

Muulize, uhusiano wako wa mwisho ulikuwaje. Je, una kitu gani unaweza kunisaidia? Una kitu gani unapenda kutoka kwangu, ukiachilia hivi vyote nilivyo navyo? Ni muhimu kufahamu mambo kama haya ili yakusaidie.

Ndoa nyingi leo zimevurugika kutokana na wanandoa kusalitiana. Mwanamume anagundua ujumbe kwenye simu ya mkewe ukiashiria kuwapo uhusiano nje ya ndoa. Mgogoro wa ndoa unaibuka.

Mwanamume naye ili kumkomoa mkewe anatafuta mchepuko eti ngoma iwe droo. Usaliti unaweza kusababisha mtu kuamsha mgogoro mkubwa hadi kubomoa kabisa ndoa.

Jambo lingine ni uzembe. Kuna wakati mwingine watu husema umri si hekima bali ni namba. Kwa hiyo unaweza ukawa mzembe kweli kweli. Na hiyo ni tabia unayoitengeneza kisaikolojia.

Unakuwa na ile hali ya kufanya vitu pasipo kutumia uwezo wako wote.

Yaani unasema bora liende. Atasema nimemaliza ile kazi lakini hajatumia nguvu zake zote. Hebu msomaji wangu nikushauri kitu kimoja; hivi itakuwaje leo ukienda kufanya kazi kwa kutumia uwezo wako wote ulio nao au ukianza kufanya kazi kwa juhudi zako zote, nini kitatokea?

Naamini yatakuwa matokeo makubwa. Hatimaye utashangaza watu wengine. Hakika, Maisha Ndivyo Yalivyo! Pengine haujawahi kutumia uwezo wako wote, sasa acha uzembe kwenye maisha yako binafsi.

Kadhalika acha uzembe kwenye kazi za watu ili kuepusha migogoro. Hiyo ni kwa sababu mwisho wa siku unaweza kukwaza watu wengine na kusababisha hali ya sintofahamu kwenye maisha ya watu wengine.

Kwenye uzembe hakikisha unapanga mambo yako kwa utaratibu. Jambo la kushangaza huwa nakaa na kufikiri sana Mungu alivyokuwa wa utaratibu katika uumbaji wa vitu vyake vyote. Alijipangia siku fulani nitaumba kitu fulani na ikawa hivyo. Ni mfano mzuri tungeweza kuutumia jinsi Mungu alivyokuwa na mpangilio mzuri. Panga mambo yako, acha uzembe, furahi na ujipongeze.

Jambo lingine linaloanzisha migogoro ni hofu. Wako watu wengi wanateseka na hofu. Hivi ni kwa nini unaogopa? Je, unaogopa kwa sababu unafikiri? Wanasema kwamba kisaikolojia ubongo unafanya kazi kuliko macho yako. Ndio maana hata watu ambao hawana uono au hawaoni, wanao uwezo wa kufanya vitu vikubwa.

Kama wewe unamwona wenzako hapo ulipo na una ubongo, basi hakikisha unabadilika na kuacha kabisa kuwa hivyo ulivyo. Hofu uliyo nayo umeitengeneza mwenyewe kwani hukuzaliwa na hofu.

Kwamba nimeitwa niende sehemu fulani sijui nitaweza! Nikiwa kwenye mkutano mmoja, kijana akapewa nafasi ya kuzungumza. Akaulizwa; unaweza kufanya nini? Akasema naweza kuchekesha lakini alipofika mbele akasema hajajiandaa.

Si kweli hakuwa amejiandaa, bali hofu kwamba atafanya nini. Alipaswa kufanya kitu watu wacheke. Kilichotokea ni hali aliyoitengeneza kichwani asifanye mambo makubwa.

***Niishie hapa ila usikose sehemu ya mwisho ya mada hii. Una maoni? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Machinga wameondolewa, sasa tupewe tafsiri sahihi

KAZI ya uondoaji wa wafanyabiashara wadogo, maarufu kama machinga, imefanikiwa kwa kiasi fulani kwenye miji na majiji mbalimbali na sasa vibanda vya muda na vya kumudu vilivyokuwa vinamea kama uyoga kwenye mitaa na barabara sasa vimepungua.

Baadhi ya miji na majiji yameongeza muda wa wafanyabiashara waliosalia kuhakikisha wanaondoka kwenye maeneo hayo kwenda walikopangiwa au kwenda kwingine kwa kuwa wengi wanafanyabiashara maeneo yasiyoruhusiwa.

Nazipongeza mamlaka zilizotekeleza suala hili kwa usahihi pia zilizoagiza kuanza kuchukua hatua dhidi ya machinga kwa kuwa kasi ya watu kukimbilia mjini na kufanya biashara maeneo yasiyoruhusiwa ilikuwa kubwa. Niliwahi kuandika katika safu hii kuwa suala la machinga likiendelea kutumiwa kama turufu ya kisiasa hatutaisaidia nchi zaidi ya kuiumiza kwa kuwa idadi yao itaongezeka na hawalipi kodi.

Baadhi ya maeneo kama Kariakoo, ilifika wakati wenye maduka walishindwa kuuza bidhaa kwa kuwa bidhaa walizo nazo machinga wanaziuza mbele ya maduka yao hakukuwa na njia ya kupita kwa watembea kwa miguu wala magari.

Kwenye vituo vya magari idadi ya vibanda iliongezeka kiasi cha baadhi ya barabara tangu mwanzo hadi mwisho kila palipo na watu vimewekwa vibanda, hali iliyopoteza mwonekano wa mji, ukaonekana mchafu na hauna mpangilio.

Mathalani, bomoabomoa ya kwanza ilianzia Barabara ya Nyerere ambayo idadi ya machinga iliongezeka na mbaya zaidi wanasiasa waliitumia kama turufu ya kupata kura kutoka kwa kundi hilo kwa kuwaaminisha kuwa hakuna wa kuwagusa, hivyo waendelee kufanya biashara zao.

Kwa sasa ukitembelea baadhi ya maeneo Dar es Salaam unaweza kupotea kwa kuwa palikuwa na vibanda vingi na sasa kuna mwonekano mzuri ambao unapaswa kuwa hivyo kila wakati ili kuepuka kukosekana kwa mpangilio maalum.

Kazi kubwa iliyopo ni namna gani maeneo hayo yatakuwa endelevu, kwamba isiwe ni zima moto bali kuwe na mikakati kuhakikisha maeneo husika yanabaki yalivyo na katika mwonekano mzuri.

Machinga waliongezeka kiasi cha kuwa hadi maeneo ambayo kwa miaka mingi hawakuwahi kuthubutu kuweka vibanda vya biashara ilifika wakati eneo la Posta kulikuwa na vibanda vingi vya machinga.

Niliwahi kuandika hapa kuwa ni lazima machinga waelezwe ukweli, wasitumike kama mtaji wa kisiasa bali waambiwe eneo fulani hairuhusiwi kufanya biashara. Ikizoeleka hivyo na wakawa kwenye maeneo fulani wateja watafuata bidhaa huko waliko na miji itabaki kuwa safi na yenye mpangilio.

Ukitaka kuiona vyema Dar es Salaam na miji mingine ni wakati uko angani kwenye ndege inayopaa au inayotua. Hapo utauona mji au jiji limepangika kiasi gani na wageni wengi ambao wanatuletea fedha za kigeni wanatumia usafiri wa anga, hivyo hujionea kulivyo.

Nchi nyingi hasa zilizoendelea zimejitahidi kusimamia mipango miji kiasi kwamba huwezi kukuta machinga kila mahali, mathalani kuzitaja kwa uchache nchi za Afrika zilizofanikiwa kuweka safi miji na majiji yake ni Kenya, Zambia, Zimbabwe na Afrika Kusini.

Katika nchi hizo unapotua au kupaa kwa ndege utajionea mpangilio wa jiji na hutaona machinga wakiwa kokote hadi karibu na uwanja wa ndege.

Kama wengine wameweza na bado wakapata wapigakura, basi hata Tanzania inawezekana. Ni lazima utaratibu uwepo huku jitihada za kuongeza ajira na mazingira ya kujiajiri yakiimarishwa.

Lakini ni muhimu kutambua kuwa uwepo wa machinga wengi mataani ni kipimo tosha cha uhaba wa ajira na hali ya maisha ya watu, na ikiwa wataongeza kipato watafungua biashara zitakazolipa kodi.

Tunavyoendelea kuwa na machinga wengi tunapunguza wigo wa walipa kodi kwenye biashara. Lazima wachache wanaolipa kodi walindwe huku machinga wakipangwa, na wale wanaokuwa kibiashara wapande daraja na kuwa kundi la walipa kodi kuliko miaka yote kubaki machinga.

Pia ni muhimu kuwa na tafsiri sahihi ya machinga ni nani,ana mtaji wa kiasi gani na biashara yenye ukubwa gani kwa kuwa ni kawaida kuona mtu ana duka dogo lakini anajiita machinga au bidhaa zilizopo kwenye kibanda chake ni sawa na zilizopo dukani lakini halipi kodi yoyote.

Kukiwa na tafsiri sahihi itaeleweka na itaisaidia nchi kuongeza walipa kodi badala ya kuongeza machinga.

# HARUSI







Ulikuwa ni usiku wa ndugu, jamaa na marafiki kumpongeza Jackline Yeuda, baada ya kufunga pingu za maisha na Siegfried Schroer. Sherehe hii ilifanyika Oktoba Mosi, katika ukumbi wa PSSSF Mawasiliano Tower Ubungo, mkoani Dar es Salaam.





# MITINDO







## Hivi ndivyo wanawake wanavyotamba mjini na kivazi hiki

MAGAUNI ya 'loose' ni mtindo mpya wa mavazi ambayo yanawasitiri wanawake wanene na wajawazito.

Mtindo huu unawafaa pia wanawake wa aina zote na unaweza kuvaa hata baada ya kujifungua. Pia ni mizuri kwa watu wanene na wale wasiopenda nguo za kubana.

Mtindo huu umebamba zaidi kwa wanawake wa ki-Afrika ambao asilimia kubwa wana asili ya miili mikubwa.

Kupitia mtindo huu wanawake huwa huru, hutembea kwa kujiamini kwa kuwa huyavaa mahali popote.

Mtindo huu wa mavazi unaweza kutumia kitenge, kanga au kitambaa cha aina yoyote na hata gharama za mishono yake ni nafuu. Mtindo huu pia unaweza kuvalia viatu vya aina zote, virefu, vifupi, vya wazi na hata raba.

Kutokana na kushamiri kwa mtindo huu tumeshuhudia hata nguo mpya zinazozalishwa nje ya nchi zikiwa za aina hiyo.



## UREMBO



# Maajabu ya kurejesha urembo wa kucha



KUCHA safi na zenye mvuto humfanya mwanamke ajiamini, aonekane mtanashati na kumwongezea ujasiri mbele za watu.

Urembo wa kucha ni muhimu kwa wanawake na wanaume kwa sababu kucha huakisi uhalisia wa mtu, kama ni msafi au mchafu.

Wanawake wengi wamejikuta wakibandika kucha ili kufunika ubaya wa kucha zao halisi.

Wengine wamekuwa wakiharibikiwa na kucha kwa kupoteza rangi yake nyeupe kwa sababu tu ya kupaka rangi.

Katika safu hii, tunaelekezana namna ya kutunza kucha zinazokatika, zenye rangi mbaya na zile ambazo hazina mvuto.

**MAHITAJI**

Dawa ya mswaki, 'baking soda', limao, maji ya uvuguvugu, mswaki au brashi na mshumaa.

**JINSI YA KUFANYA**

Chukua dawa ya mswaki changanya na unga wa 'baking soda' kisha weka kwenye kucha zako. Sugua na mswaki mpaka uone uchafu unatoka.

Ukiona zimeanza kutakata nawa mikono yako kwa maji ya uvuguvugu, kisha futa na taulo na paka mafuta ya Olive au yoyote ya mkononi.

Njia nyingine ni ya kutumia limao na 'baking soda'. Kata kipande cha limau kikamulie kwenye bakuli kisha weka unga wa 'baking soda' kiasi na changanya mpaka upate uzito wa kukuwezesha kutumia kusugulia kucha zako.

Baada ya hapo, chukua mswaki, chovya mchanganyiko kisha sugua kucha zako mpaka uone zinatakata na suuza na maji ya moto kisha upake mafuta ya olive (mafuta ya mzeituni).

Ukimaliza kusafisha kucha zako, chukua maji ya mshumaa na dondosha matone yake juu ya kucha kisha acha kwa dakika tatu hadi upoe kabisa.

Maji ya mshumaa yanafanya kucha zako ziwe ngumu na imara, zisikatike na kukua vizuri na zenye afya.

Unaweza kurudia kuchoma kucha zako mara kwa mara hadi utakapoona zimekuwa ngumu na zinazostahimili maji.

## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Namna ya kutengeneza mkate bora wa mahindi







MKATE wa mahindi una ladha tamu, harufu nzuri na huliwa wakati wowote.

Mapishi haya yanajumuisha maziwa, 'butter' na asali ambayo huufanya mkate kuwa mtamu na wenye kuvutia zaidi. Ni pishi unaloweza kuandaa ili kuipa familia yako ladha nzuri.

**MAHITAJI**

Sukari nyeupe kikombe kimoja, unga wa mahindi kikombe kimoja na nusu, ngano nusu kikombe, 'baking soda' nusu kijiko cha chai, chumvi nusu kijiko cha chai, 'butter' nusu kikombe, 'butter' ¾ kikombe, asali vijiko vitatu vya chai, maziwa kikombe kimoja na robo, zabibu kavu nusu kikombe na mayai manne.

**NAMNA YA KUANDAA**

Bandika sufuria jikoni, weka 'butter' (¾ kikombe), acha iyeyuke. Ipua kisha weka sukari na mayai kwenye sufuria. Koroga pamoja hadi vilainike vizuri. Changanya 'baking soda' na maziwa kisha weka kwenye bakuli lenye mchanganyiko wa mayai na koroga kwa pamoja vizuri.

Weka unga wa mahindi, unga wa ngano na chumvi kwenye bakuli yenye mchanganyiko wa mayai.

Changanya vizuri mpaka mabonge yapotee na mchanganyiko uwe laini wastani.

Weka asali na zabibu kavu kwenye bakuli yenye mchanganyiko wa unga. Changanya vizuri kisha weka mchanganyiko kwenye chombo unachotumia kuokea.

Tega muda kati ya dakika 30 hadi 40 na hapo mkate utakua tayari.

Ipua mkate kisha paka vizuri nusu kikombe cha siagi juu ya mkate ili kuupa ladha tamu zaidi. Acha upoe utakuwa tayari kwa ajili ya kuliwa na chai, soda au kinywaji kingine.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# King'arishe kitanda chako chumbani

USAFI wa kitanda ni jambo linalopaswa kufanywa kila siku katika nyumba.

Pia hufanywa muda wowote kwa kutegemea matumizi yake ilimradi chumba kionekane kisafi wakati wote, kwa sababu ni miongoni mwa vitu vinavyochangia kung`arisha nyumba.

Msingi mkubwa wa usafi wa kitanda hiki huanzia asubuhi unapoamka. Usafi ninaouzungumzia hapa ni kuanzia kutandika mashuka, kufuta vumbi pande zote zinazokizunguka chumba na kukipangilia vizuri.

Shuguli hizo zote ili zifanikiwe kwa umakini na ustadi zaidi, zinapaswa kufanyika muda mfupi baada ya kuamka na si vinginevyo.

Uzoefu unaonyesha kwamba mtu anapoamka na kuanza kutandika kitanda bila kuchelewa ama kufanya shuguli za nyumbani anaweza kufanya vizuri zaidi kuliko akisubiri kwanza afanye usafi wa kinywa.

Na hata kama akifanya baadae anaweza asifanye kwa umakini ama ustadi zaidi kama anapoamua kufanya hivyo muda mfupi baada ya kuamka.

Kwa sababu kitanda ni moja ya vitu vinavyoifurahisha nafsi katika nyumba na kiafya pia, ni vizuri kikapewa kipaumbele kikubwa.

Pia ili nafsi yako ifurahi kweli na kukusaidia upendelee kuwapo nyumbani mwako kuburudisha macho, kuna umuhimu wa kuhakikisha unakitendea haki kitanda kwa kukifanyia usafi na kukitandika vizuri.



Kinachohitajika zaidi hapa ni ubunifu au umaridadi kwa lugha nyingine na kuweka ubunifu zaidi. Kwa mfano, kama uwezo wako unaruhusu si vibaya pia mashuka yako unayotandika kwenye kitanda yakaendana na mapazia yako. Hii ni kwa ajili tu ya kuking`arisha zaidi chumba chako. Kama umetandika shuka la pinki, basi inafaa mapazia yako yakashabihiana na rangi za mashuka.

Inawezekana ukatenganisha shuka unalotumia kulalia na ambalo unalitumia katika shughuli hiyo ya kutandika, hapo uwezo wako kiuchumi ndio utaamua.

Pia kuna mbinu nyingi za kukifanya kitanda chako kiwe katika hali ya usafi na mvuto wa kipekee na uepuke kukiacha kichafu hata kama si kwa kufuata hayo niliyasema.

Kumbuka kila kitu kinahitaji ubunifu. Jitahidi kuongeza ubunifu kila siku kutafuta namna bora ya kukifanya kitanda chako kipendeze kwa sababu lengo kubwa ni kukipendezesha chumba kwenye nyumba yako, nafsi na ustawi wa afya yako pia.

## Jinsi ya kuchagua mitungi ya mapambo



WATU wengi wanapenda nyumba zao zipendeze, na moja ya vitu vinavyong'arisha ni mitungi ya mapambo. Zifuatazo ni dondoo za kichagua mitungi ya mapambo.


**1:** Hakikisha unachagua mitungi yenye rangi nzuri kulingana na mandhari ya nyumba.

**2:** Chagua yenye maumbo ya kuvutia ambayo mwonekano wake utawashangaza watu.

**3:** Chukua mitungi yenye viambata kama vile mchi, mnyama au beseni la maji.

**4:** Angalia aina ya udongo uliotengeneza mitungi, hakikisha ni imara na uliochanganywa na saruji kidogo.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
'GRRRRRR!!!
'GRRRRR!!!
UKATILI
NDOA
!
KUNA MTU KANIPIGIA KASEMA ANAKUJA OFISINI KUNIPA 'UBUYU' NIMEKATAA
KWA AKILI YAKO ULIDHANI UBUYU WA KUMUNG'UNYA! UJUI KUWA KISWAZI UBUYU NI UMBEA!
MGONJWA UNA-SOMA GAZETI?
HAPANA! NASONGA UGALI NAKARIBIA KUPAKUA
TRANS
SHIKAMOO AFANDE...
SIO DAWA
POLE SANA UTA-RUHUSIWA LEO... TUPE MAONI YAKO KILICHOKUVUTIA HAPA KWETU
VIMINI VYENU HADI NAJIHISI NIPO KASINO SIO WODINI
MZEE KUMBUKA UNATAKIWA KUFA UNAVYOZIDI KUGANDA DUNIANI NASHINDWA KUUZA HII NYUMBA!
DUH!
MWANAUME KUJIAMINI AU SIO?
KWA WAKE ZA WATU?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...MWENYE NJAA HACHEKI

HABARI KIMATAIFA

# Urusi na china zafanya doria ya pamoja Pasifiki

**MOSCOW,** URUSI

Meli za kivita za Urusi na China zimefanya doria ya kwanza ya pamoja ya kijeshi katika eneo la Magharibi la bahari ya Pasifiki.

Ikithibitisha habari hizo Wizara ya Ulinzi ya Urusi ilisema doria hiyo ilianza Oktoba 17 hadi 23.

Serikali za Moscow na Beijing, ambazo zilifanya mazoezi ya pamoja katika eneo la bahari ya Japan mapema Oktoba, zimezidi kuimarisha uhusiano wa kijeshi na kidiplomasia katika miaka ya hivi karibuni, katika kipindi ambacho pia uhusiano wao na mataifa ya Magharibi ukiwa umevurugika.

Operesheni hiyo ya kijeshi imekuwa ikifuatiliwa na Japan ambayo mapema wiki hii ilisema kundi la meli 10 kutoka China na Urusi zimeonekana zikipita katika bahari wa Tsugaru, ambao unaigawa Japan Bara na kisiwa chake cha kaskazini cha Hokkaido.

Wizara ya ulinzi ya Urusi imesema doria hiyo ina lengo la kudumisha amani na utulivu katika eneo la Asia-Pasifiki na uangalizi wa shughuli za kiuchumi katika eneo la bahari baina ya mataifa hayo mawili.

DW

# Merkel ahimiza wanawake kushiriki zaidi katika siasa

**BERLIN,** UJERUMANI

KANSELA wa Ujerumani aliyemaliza muda wake, Angela Merkel, ametoa wito kwa wanawake kujihusisha zaidi na siasa.

Kauli hiyo aliitoa katika toleo la mwishoni mwa wiki katika gazeti la Sueddeutsche. Mwanasiasa huyo wa chama cha Christian Democrat (CDU) alisema kuwa wanaume pekee kwenye siasa si jambo linalokwenda na wakati.

Alisema kwa vyama vya siasa kuwakilisha umma kikamilifu, vinapaswa kuzingatia usawa wa kijinsia ili kutimiza wajibu huo.

Kambi ya kansela huyo ya vyama ndugu vya CDU/CSU ilipata anguko la kihistoria katika uchaguzi wa shirikisho la Ujerumani ambao ulihitimishwa mwezi Septemba.

Merkel, ambaye ni kansela wa kwanza mwanamke, yupo katika hatua ya kujiweka chonjo na siasa baada ya miaka 16 ya uongozi wake wa Ujerumani.

DW

# Mashambulizi jeshi la Ethiopia yazuia ndege ya misaada kutua

**ADDIS,** ABABA

MASHAMBULIZI ya anga ya Jeshi la Ethiopia katika mji mkuu wa Jimbo la kaskazini la Tigray, yamesababisha ndege ya misaada ya Umoja wa Mataifa kushindwa kutua mjini Mekelle.

Kwa mujibu wa taarifa ya Ofisa Mratibu wa Misaada ya Dharura wa Umoja wa Mataifa, Martin Griffths, tukio hilo lilitokea jana, Ijumaa na kwamba ndege husika ilirejea mjini Addis Ababa.

Griffths aliongeza kwa kusema tukio hilo linaongeza wasiwasi mkubwa kuhusu usalama wa wafanyakazi wenye dhima ya kutoa misaada ya kiutu katika kusaida raia wenye uhitaji.

Hata hivyo Umoja wa Mataifa ulikuwa na kibali cha safari ya ndege hiyo na haukupata tahadhari ya onyo la mashambulizi ya Makele. Takribani mwaka mmoja tangu kuanza kwa mzozo wa Tigray, watu 400,000 wanakabiliwa na kitisho kikubwa cha njaa, katika eneo hilo la kaskazini mwa Ethiopia.

DW



Sehemu ambayo imeathirika na shambulio la angani la serikali na kusababisha Ndege ya misaada ya Umoja wa Mataifa kughairi kutua Ijumaa huko Mekele, mji mkuu wa Jimbo la Tigray. **Picha BBC.**

# Mvulana auawa katika shule ya wasichana

**NAIROBI,** KENYA

MVULANA mmoja mwenye umri wa miaka 17 kutoka Kenya, amefariki kutokana na majeraha aliyopata wakati aliposhambuliwa baada ya kuingia kisiri katika shule ya wasichana, polisi wamesema.

Mwanafunzi huyo wa kidato cha nne alikuwa miongoni mwa wanafunzi sita ambao waliripotiwa kuingia kinyemela katika shule ya wasichana kaunti ya Kiambu ambayo ni jirani na mji mkuu wa Nairobi. Maofisa wa polisi wanasema kwamba mwanafunzi huyo aliingia katika bweni la shule hiyo muda wa saa kumi alfajiri kabla ya kuonekana na baadhi ya wasichana ambao walipiga kelele.

Hatua hiyo iliwavuta walinzi wa shule hiyo , wafanyakazi na mwalimu mkuu. Wavulana watano kati yao walitoroka, kwa mujibu wa maofisa wa polisi aliyesalia alivamiwa na wanafunzi na wafanyakazi wa shule hiyo.

"Walimpiga na kumfanya kupata majeraha ambayo yalitishia maisha yake. Mvulana huyo baadaye alifariki", idara ya jinai ilisema katika mtandao wake wa twitter.

BBC

MAKALA

# MABANGO KWENYE MIKUTANO YA RAIS



Na Magabilo Masambu

**Utaratibu wa mabango kwa hapa kwetu na hasa mabango kwenye mikutano ya Rais, unaweza kuwa na tafsiri nyingi ambao kwangu siutazami tu kwa maana moja ya kuwasilisha hoja, kero, matatizo au aina yoyote ya ujumbe kwa viongozi au kwa Rais mwenyewe.**

KWA mujibu wa maelezo mbalimbali, neno bango lina maana ya karatasi au kitambaa kilichoandikwa ujumbe mfupi, wenye kukusudia kutoa habari au tangazo fulani kwa hadhira. Naweza kusema ni nyenzo inayotumiwa na fanani kufikisha ujumbe kwa hadhira.

Utamaduni wa kutumia mabango katika kutoa habari umekuwapo duniani katika kutangaza biashara au kufikisha ujumbe kwa viongozi wa serikali, hivyo si jambo geni.

Lakini hapa kwetu Tanzania, utamaduni huu si wa miaka mingi kwa wananchi kutumia mabango kuwasilisha hoja zao kwa viongozi.

Naweza kusema utamaduni wa mabango hasa yale yanayotumiwa na wananchi kufikisha ujumbe au kero zao kwa viongozi wakuu wa serikali, umeanza miaka michache iliyopita hasa katika uongozi wa awamu ya tano ya serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Utaratibu wa mabango kwa hapa kwetu na hasa mabango kwenye mikutano ya Rais, unaweza kuwa na tafsiri nyingi ambao kwangu siutazami tu kwa maana moja ya kuwasilisha hoja, kero, matatizo au aina yoyote ya ujumbe kwa viongozi au kwa Rais mwenyewe.

Marehemu baba yangu akiwa hai, kila wakati alikuwa akiniambia kwamba: "Wewe ndiwe kijana wangu mkubwa. Nikiondoka mimi wewe utakuwa kiongozi wa familia hii, kwa hiyo ni jambo la aibu sana kama wadogo zako watafanya makosa mimi nikagundua wakati wewe upo hapa na hujui."

Kuna wakati nayakumbuka sana maneno ya baba yangu.

Sababu moja kubwa ni kwamba baada ya yeye kufariki dunia ni kweli mimi ndimi nimebaki kama kiongozi wa familia yetu na nafurahi sana kuona tangu aondoke, familia yetu imeendelea kuwa na umoja ule ule. Mimi na wadogo zangu tunaishi kwa kushirikiana kwa upendo kwa sababu nilijifunza kuiongoza familia kabla baba yangu hajaondoka duniani na ninajivunia hilo.

Ni kweli kwamba wananchi wanayo matatizo lakini serikali inao mfumo kutoka Rais mpaka kiongozi wa chini kabisa labda balozi wa nyumba 10. Lakini kwa nini wananchi wanapenda sana awapo Rais mahali ndipo iwe nafasi ya kupeleka matatizo yao? Kuna mahali tumetengeneza tatizo bila kujua.

Ni hatari sana wananchi kuamini au kuaminishwa kwamba mtu pekee anaeweza kutatua matatizo ya nchi hii ni Rais pekee.

Hatari zaidi ni wananchi kutokuwa na imani kwamba watendaji wa serikali ngazi ya chini kabisa, ambao wengine wamewachagua wenyewe au wameteuliwa na Rais, hawawezi kuwasaidia kwa lolote.

Nimetoa mfano wa marehemu baba yangu yeye alikuwa kama Rais nami nikawa mtendaji wake.

Wadogo zangu walijua hivyo kwamba tukipata tatizo tunamwambia kaka, anayoweza kutatua, atataua na anayoshindwa basi atazungumza na baba.

Si vibaya kumshukuru Rais kwa mambo anayoyasimamia kama kiongozi mkuu wa serikali lakini si vyema vilevile kuona kila jambo linalofanyika katika serikali ni Rais kafanya badala ya serikali imefanya ambayo ni viongozi wote pamoja na wananchi wenyewe.

Ndiyo maana leo hata katika mahakama zetu, uamuzi fulani ukitoka lazima Rais anahusishwa. Ukiwa mzuri shangwe na vigelele kwa Rais na kwamba anaupiga mwingi sana, ukiwa mbaya kutegemea ni uamzi juu ya nani Rais ni mbaya sana!

Hii dhana isipokufa, tutakuwa na taifa la ajabu sana huko mbeleni. Pengine ni mifumo yetu ya kisheria ambayo nadhani kama iko hivyo, basi yanahitajika marekebisho ya haraka sana, ili mtazamo wa kitaifa uwape imani wananchi kwamba wao ndio wanaliongoza taifa lao na Rais ni msimamizi wa shughuli zao za maendeleo.

Jambo hili nafikiri linawapa tabu sana viongozi wa ngazi za chini na hasa Rais Samia Suluhu Hassan alipotangaza kwamba hataki kuona mabango kwenye mikutano yake.

Naamini hakuwa na lengo baya, alimaanisha viongozi wa chini washughulike na matatizo ya wananchi lakini hilo halitawezekana kama tu wananchi wanaimani kwamba anayestahili kutatua matatizo yao ni Rais pekee.

Tutarudije kwenye imani kwamba serikali ndiyo inafanya akiwamo Rais mwenyewe. Simfundishi Rais kufanya kazi, lakini yeye ndiye mwenye kuiondoa hali hii kwa kuonyesha kwamba wananchi ndio wanafanya kila kitu na faida yake kubwa kabisa. Wananchi wakishakuwa na imani kwamba nchi wanaijenga wao uzalendo wao kwa nchi utakuwa mkubwa sana.

Hata haya malalamiko ya tozo yanakuja kwa sababu wengi wanaamini hizo pesa wanawachangia watu wengine na kwamba wao wako pembeni.

Tulishinda vita vya Uganda dhidi ya Idi Amin Dada si kwamba Mwalimu Julius Nyerere alikuwa na nguvu sana la hasha!

Tulishinda kwa sababu wananchi walijiona sehemu ya taifa na taifa sehemu ya wananchi, ndiyo maana wengi walijitolea mali zao hata bila kuambiwa kwa sababu waliona nchi ni yao na wao ni sehemu yake.

Wananchi wakishakuwa na imani hiyo kwamba nchi wanaijenga wao, viongozi wa ngazi za chini pia wakafungua milango yao kuwasikiliza, hakika hamtaamini juu ya ushirikiano mkubwa wa wananchi kwa serikali na hayo mabango hayataonekana kabisa kwenye mikutano ya Rais.

Ushirikiano baina yao na viongozi wa chini utakuwa mkubwa sana. Kinyume chake, viongozi hawa watalaumiwa bure na hawatazuia mabango kwenye mikutano kwa au kuwatishia wasiandike kwa sababu mtatizo ni ya kila siku.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Mdundiko ulivyokuwa unapoteza watoto



Na Adam Fungamwango

LEO tuko kwenye maeneo ya Pwani, kama vile Dar es Salaam, Bagamoyo, Kisarawe na Kibaha ambako kulikuwa na ngoma maarufu ya mdundiko.

Ilikuwa ngoma maarufu sana miaka ya 1980 hadi 1990. Hadi leo ipo lakini imepungua nguvu na umaarufu hasa sehemu za mijini, hususan Dar es Salaam.

Ngoma hii ilikuwa maarufu sana kwenye sherehe za kiserikali na kijamii, kama vile harusi, jando, kipaimara, komunio na hata wakati wa hafla za viongozi wanapotaka kuhutubia.

Ni ngoma ya asili ya Wazaramo wa mikoa ya Pwani na Dar es Salaam, ambayo miaka niliyoitaja ilikuwa ikipita sehemu, inazoa idadi kubwa ya watu na kuondoka nayo hadi itakapokwenda kufikia.

Wapigaji walikuwa na ngoma kubwa ambayo ndiyo kinogesho cha ngoma yenyewe. Inafungwa kamba ambayo mpigaji anaivaa mabegani kwa sababu ni kubwa na nzito. Kuna mpiga debe, halafu mpiga manyanga, ngoma moja ndogo inayopigwa pande zote mbili kwa kutumia mkono maarufu kama 'kidalidali' pamoja na vitatarizi vingine ambavyo wenyewe wataona vinafaa.

Wengi waliokuwa wanasombwa na ngoma hiyo ni wanawake na watoto. Staili ya ngoma hii haikai sehemu moja. Ni ngoma inayotembea. Inaweza kutoka Ilala ikaenda hadi Msasani au Mbagala hadi Buguruni. Inakatiza barabara na mitaa yake. Kila inapopita, kinamama wanatoka majumbani mwao ili kuangalia, kucheza au kuondoka nayo moja kwa moja wakicheza na kuburudika. Watoto nao ni hivyo hivyo.

Itoshe kusema tu kuwa ilikuwa inachukua umati mkubwa na watu kiasi kwamba unaweza kupotezana na mtu hapo hapo kwenye ngoma na usimwone tena, hapa umtafute vipi.

Kwa kiasi kikubwa ilikuwa inaleta burudani kwa jinsi wanavyoipita, wanavyokatiza mitaa huku kukiwa na kundi kubwa la watu mara 10 la hawa wa sasa wa kigoma cha 'Uruguay', 'mduara' au 'kigodoro'. Aina ya uchezaji wa kinadada wa wakati huo, ilikuwa wakisakata huku wakizurura nayo.

Awali sikuwa najua ni kwa nini mdundiko huwa unatembea na haukai sehemu moja kama ngoma zingine. Lakini baadaye nilipokuja kuwa mkubwa kidogo, niligundua kuwa kumbe ngoma hiyo ilikuwa inakodishwa na kule kutembea ni kwamba wapiga mdundiko walikuwa wakitoka kwenye makao makuu yao na kwenda kule walikokodishwa, iwe kwenye sherehe, mkutano au hafla.

Na hata wakati wa kurudi kwao pia walikuwa wakipiga na kutembea, kutoka walikoalikwa baada ya kumaliza sherehe. Kwa wakati ule vikundi havikuwa vingi sana, baadhi yao kulikuwa na 'Kikundi cha Taifa', 'Joka Kuu' na vingine vichache. Hata hivyo, mahitaji yalikuwa makubwa, hivyo kinamama wa Kinondoni wakienda Buguruni kukodisha wao hawaweki ngoma zao mabegani hadi wafike eneo husika au kukodishiwa magari kama hawa wa sasa, la hasha.

Wanaanza kupiga kuanzia hapo hapo kwenye makao makuu yao na kuanza kuondoka na akinamama wahusika waliowakodisha, iwe wawili au watatu hadi Kinondoni. Sasa huko njiani ndiyo balaa. Kila wanapokatiza wanapata watu wa kuondoka nao. Vijana wa mjini wa sasa wanasema 'wanasepa na kijiji'.

Hadi wafike kwenye sherehe mdundiko unakuwa umepeleka idadi kubwa ya watu ambao hawajaaalikwa. Kizuri ni kwamba zamani hakukuwa na kadi wala barua ya mwaliko. Yeyote yule anayekuwapo ndiye mwalikwa. Na kwa uchunguzi wangu mdogo niligundua kuwa wanapofika kwenye sherehe, hafla, au mkutano haipigwi tena staili ile ya mdundiko.

Wanapokuwa wamekaa chini wanapiga staili au ngoma ya vanga na si mdundiko tena. Nadhani ilionekana utamu wa ngoma ya ndundiko ni kule kutembea kwenyewe na kukatiza mitaa na barabara.

Pamoja na burudani ya aina yake, kuna athari zilikuwa zikipatikana kutokana na ngoma hiyo. Nayo ni kupotea kwa watoto. Pia ni wanawake kuunguza mboga na wakati mwingine kuingia mzozo na waume wao, ikiwemo kupigwa.

Watoto waliipenda sana ngoma hiyo. Na kila ikipita ni lazima wanganishe na kuzurura nayo. Tatizo wanapochoka na kujitoa kwenye kundi, wakajikuta wapo mbali na nyumbani, na hawajui njia waliopitia hadi kufika hapo. Kifupi tu ni kwamba wanakuwa wamepotea. Hata wale wanaofika mwisho kwenye sherehe, pia wanakuwa hawawezi kurudi walikotoka. Wazazi wanapata shida ya kuwatafuta. Hadi kupatikana ni lazima kazi kubwa ifanyike, au vituo vya polisi vihusike. Wakati huo simu hakuna.

Kwa upande wa kinamama hao hawapotei. Tatizo ni kwamba wakati mwingine wanakuwa wamebandika mboga, nyama au maharagwe. Mdundiko unapita. Anakimbilia, anacheza au kufuatana nao kwa robo, nusu au kilometa moja. Akirudi nyumbani mboga imeungua.

Pata picha mumewe akirudi inakuwaje. Wakati mwingine hata kama hajaacha mboga jikoni, akirudi anamkuta mumewe amesharejea kazini. Nyumbani hakukuta mtu. Mke hata akijitetea alifuata ngoma, bado itaonekana ni tatizo. Kwani wakati mwingine mama amefuata ngoma mlango ameacha wazi.

**Kwa maoni 0716 350534**

# HADITHI

# Ajenda ya Siri-1

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote i kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Taabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia darasa la saba tu. Alipofisha umri wa miaka 18, alikimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabishara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki dunia kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je, ni wafanyabishara wenzake Chilambo ndio waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

MAHAKAMA imesikiliza ushahidi wa pande zote mbili. Upande wa mashtaka uliongozwa na Wakili Heri Seif na mashahidi mbalimbali akiwemo mke wa marehemu, Hellen Kisa, daktari aliyechunguza mwili, Thomas Mtuta, na mfamasia Mwahija Chota.

Pia umesikiliza upande wa utetezi, akiwamo mtuhumiwa mwenyewe, Tina Kauzeni. Upande wa mashtaka umethibitisha kuwa kwa maelezo ya mdomo na ushahidi wa vielelezo, mtuhumiwa aliimuua Hafidh Chilambo kwa kumwekea aina mbili za vidonge kwenye chakula ambavyo vikichangaywa na kuwekwa idadi isiyohitajika inakuwa sumu inayoweza kuumuua mtu kwa saa mbili baada ya kunywa. Kutokana na hilo, Mahakama inamhukumu mtuhumiwa adhabu ya kunyongwa hadi kufa.”

Ilikuwa hukumu nzito iliyotolewa na Jaji Paul Kilongola wa Mahakama Kuu.

Kuna aina mbili za kelele zilisikika kwa wakati mmoja. Ya kushangilia hukumu hiyo ambayo ilionekana kuishinda ile ya vilio.

“Haki imetendeka, tunashukuru Bwana kwa kunyoosha mkono wako kwa mtu mwovu.” Ilikuwa sauti ya mke wa marehemu Chilambo. Baadhi ya ndugu wa mke wa marehemu, Hellen, waliungana na baadhi ya ndugu wa marehemu mumewe kushangilia, kukumbatiana na kuonyesha jinsi gani wameimaliza kazi. Kazi ya kuhakikisha mtu aliyemuua Chilambo anafikishwa kwenye mkono wa sheria ya haki inachukua mkondo wake. Walikuwa wengi mno. Walimiminika tangu asubuhi siku hiyo ya hukumu. Ndiyo siku ambayo walijaa zaidi kuliko siku nyingine yoyote.

Ni watu watatu tu ambao waliangua vilio. Walimlilia Tina. Si kwa sababu hakufanya tukio hilo, la hasha. Kwa sababu hukumu imetoka walijua kabisa kuwa Tina ameua. Hata ushadidi ulivyokuwa unatolewa moja kwa moja, walijua hachomoki. Walilia kwa sababu wanamfahamu. Waliishi naye. Kile kitendo cha kusikia kuwa anakwenda kunyongwa, kiliwatoa simanzi, huzini, huruma na imani.

Historia ya msichana huyo mdogo ambayo alikuwa anawasimulia alivyopata taabu na kuhangaika pia ilizidi kuwafanya walie kwa sauti zaidi.

“Oooh, Tina wangu miee, nitakuona wapi tena. Kwa heri Tina. Kwa heri ya kuonana. Mungu akutangulie mwanangu.” Alionekana mama mmoja wa makamo akilia zaidi kuliko wenzake. Alikuwa akibebelezwa na mwanaume mmoja wa makamo na msichana aliyeonekana ni binti yake.




> **“Oooh, Tina wangu miee, nitakuona wapi tena. Kwa heri Tina. Kwa heri ya kuonana. Mungu akutangulie mwanangu.” Alionekana mama mmoja wa makamo akilia zaidi kuliko wenzake. Alikuwa akibebelezwa na mwanaume mmoja wa makamo na msichana aliyeonekana ni binti yake.**

Mhukumiwa yeye aliangua kilio na kuishiwa nguvu baada ya hukumu hiyo. Alianguka chini. Baada ya dakika mbili ya kupata huduma ya kwanza alizinduka. Alinyanyuka, lakini hakuwa na nguvu. Alikuwa alikuwa anapepesuka.

Ghafla alimwona mama aliayekuwa analia. Akaanza kulia tena. “Kwa heri shangazi, Mungu akipenda tunaonana mbunguni.” Tukio hilo liliendela kuhuzunisha baadhi ya watu waliohudhuria mahakamani wakati wa kusomwa kwa hukumu hiyo.

Hatua chache baada ya kulifikia karandinga la kumpeleka gerezani kukaa, akisubiri siku ambayo atanyongwa hadi kufa, Tina aligeuka. Bado machozi yalikuwa yakimtiririka. Akapunga mkono wa kulia kuelekea kwa mama aliyekuwa analia na wale wawili aliokuwa nao. Aliyeitwa shangazi alikuwa hajiwezi kwa kilio, huku akiwa amekamatwa na yule baba na msichana.

Wote watatu walishindwa kumpungia Tina. Hawakuwa wakiamini na kushikwa na ganzi. Alikuwa amevaa dela lake rangi ya zambarau, sendo, akiwa amesuka msuko wa yeboyebo. Aligeuka, anavuta hatua mbili. Kama akisita hivi, halafu ananyanyua mguu mmoja na kupanda kwenye karandinga. Tayari kwenda kutumikia adhabu ya kifo ambayo amehukumiwa.

Hapo ndipo ilikuwa mwisho wa Tina kuonekana hadharani. Tayari alikuwa ndani ya karandinga.

Baadhi ya watu waliohudhuria mahakamani hapo siku ya hukumu hiyo, hawakuwa na upande. Walikuwa wanashangaa tu. Kuna walioona ni adhabu stahiki kwa msichana huyo kutokana na aina ya kifo cha mfanyabiashara huyo mkubwa lakini wako waliokuwa wakimwonea huruma msichana huyo, wakidhani ni adhabu kubwa sana kwake.

Wako waliotaka kujua sababu ya msichana huyo kufanya mauaji hayo ili walinganishe na hatua aliyoichukua. Baadhi ya watu hutaka kwanza kujua ukubwa au uzito wa kitu alichofanyiwa muuaji mpaka kufanya hivyo. Hapo ndipo wanaamua na hata kama kafanya kitu kibaya, wanaona kama hakufanya makusudi bali jazba, munkari, hasira au kisasi ndicho kimemfanya akafanye hivyo.

Sheria haiko hivyo. Inaangalia kama kosa limetendeka au halijatendeka. Inafanya hivyo kwa kupitia ushahidi wa pande zote mbili uliowasilishwa mahakamani. Haifuatilii sana kisa ili mshtakiwa au mtuhumiwa iwe sababu ya kujitetea kwake.

Wako walioona adhabu hiyo ni shahiki kabisa kwa msichana huyo kwa sababu za kisaikolojia. Baadhi yao wameshawahi kupata majanga kutokana na madada wa kazi.

Kuna mama mmoja yeye alikuwa hapo hapo mahakamani, alinyang'anywa mume kabisa na dada wa kazi.

Baada ya kumletea nyodo mumewe, akageuza kibao na kumtwaa dada wa kazi. Kabla ya dada kuolewa, akatwangwa talaka. Hadi leo hii yeye na madada wa kazi ni tofauti. Moyoni aliona ni sawa tu.

“Hawana adabu hawa. Yaani nimemtoa Dodoma hatazamiki. Nimeanza kumsafisha mwenyewe, nimempa vipodozi, kaanza kuonekana, alichoona yeye ni kunichukulia mume. Sawa sawa wakomeshwe tu hawa,” alijisemea moyoni wakati dereva wa karandinga akiwasha moto gari kwa ajili ya safari ya gerezani. Mwingine hadi leo ana makovu ya kuibiwa mtoto wake. Miaka mitatu iliyopita alimpata dada wa kazi kwa ajili ya kumlea mtoto wake wa mwaka mmoja, huku yeye akiwa mfanyakazi. Anamwacha mtoto nyumbani na dada yeye akienda kazini. Siku isiyo ya jina, hakumkuta mtoto wake wala dada wa kazi. Hadi leo hajui walikotokomea.

Huyu dada alikuwapo mahakamani. Moyoni hukumu hii ilimfurahisha sana ingawa haikufuta machungu na majonzi aliyo nayo. Si kina mama tu waliokuwa na masononeko na madada wa kazi.

Hapo hapo mahakamani kuna baba mmoja yeye alikuwa na mfanyakazi wake wa ndani, akamtaka kimapenzi. Wakakubaliana vizuri. Alichofanya ni kumsafirisha mkewe kwenda kwao baada ya kupata msiba. Akaona nafasi si ndiyo hii?

Msichana kabadilika bwana. Akakataa. Baba akataka kumbaka. Msichana akafanikiwa kuchomoka na kukimbia. Akampigia simu mkewe na kumweleza kila kitu, huku akimwambia hawezi kurudi tena nyumbani kwake. Mke alipovyorudi hala hakuwa na maneno mengi. Alichotaka ni talaka yake tu. Hakuliki hakulaliki mpaka baba wa watu katoa talaka. Hivi sasa hana hata mke. Mke hataki kurudi na hajaona bado. Huyu naye alione sawa tu.

“Ndiyo wale wale tu.” Alijikuta akimtamka maneno hayo, ingawa ni sauti ya chini sana.

INAENDELEA JUMAPILI



# SHILOLE WAPASHE WAPASHIKE

KWA sasa imekuwa ni kawaida kwa mastaa wa kike maarufu Bongo Movie, kufanya 'surgery' ili kubadilisha mwonekano wao.

Suala hili limeshika hatamu kwenye mitandao ya kijamii ambapo kila mtu anatoa maoni yake juu ya mastaa waliofanya upasuaji, ambao kuna baadhi wamechonga sura, kuweka 'dimpozi' na kupunguza matiti.

Suala hilo limemkera mwanamuziki maarufu 'Shishi' ambaye ametoa maoni yake kupitia ukurasa wake wa instagram; "

Wazungu mliosoma mtusaidie jamani alichokisema huyu dada,

"Wanawake wenzangu tujikubali na Mungu alivyotuumba. Kuna muda itabidi tukubali kuwa umri umetuacha na tukubali matokeo. Mkitaka kushindana na hawa watoto wenye vitumbo vidogo tutakufa kizembe. Maana naona safari za Uturuki zimekuwa nyingi sana ndugu zangu acheni kuiga mastaa wa nje, nyie wenzangu chai ya rangi asubuhi na kitumbua inahusu? Vibonge wenzangu Shamsa Ford tujikubali."

Anaandika Shilole.

## Chameleone akichafua upya

WABONGO wanakumbuka sana ngoma za 'Mama Rhuda', 'Teresia', 'Valuvalu', 'Tubonge' na zingine nyingi za msanii bora kabisa Afrika Mashariki, Jose Chameleone.

Kwa sasa, Mganda huyo ameonekana kupoa kidogo, lakini habari nzuri ni kwamba muda wowote ataachia albamu moja kati itakayojulikana kama 'I am Joseph'.

Mtayarishaji wake wa muziki Hannington Bugingo amedokeza wamekamilisha ngoma sita, na wako studio wakimalizia nne zilizobaki, kwani albamu hiyo inatakiwa iwe na nyimbo 10.

Ilikuwa itoke Oktoba 9, siku ya kuadhimisha Uhuru wa Uganda, lakini haikuwezekana, muda wowote sasa mashabiki wa msanii huyo Afrika Mashariki na Kati wajiandae kwani huwa hababahatishi.



## Big, hao nyuki toleo la mwisho nini?

RAPA Sean Michael Leonard Anderson alimaarufu Big Sean mwenye umri wa miaka 33 kutoka mitaa ya Santa Monica California nchini Marekani, siku ya jana alitrendi sana mitandaoni baada ya kupost picha kwenye mtandao wa Instagram akiwa amegandwa na kundi la nyuki wakati ana shuti video yake mpya ya "What A Life".

Big Sean anadai kwamba nyuki hao walikuwa Elfu 65,000 mwilini mwake.

Akaongeza kusema alikuwa na upendo kwa mzinga wa nyuki, na hataki kufikiria suala hilo kama lilikuwa na athari kwake au ujinga.

Sasa mashabiki wengi, wakiwamo Wabongo, ambao wanawajua nyuki walivyo wakorofi, wanajiuliza ni nyuki wa aina gani hao? Nyuki haumi? Nyuki wa Afrika na wa Marekani wana utofauti? Au nyuki toleo la mwisho?



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**CONTE AITAMANI UNITED**

KOCHA wa zamani wa Juventus, Chelsea na Inter Milan, Antonio Conte, "atapenda" kuchukua usukani pale Manchester United iwapo klabu hiyo ya Ligi Kuu England itamfuta kazi, Ole Gunnar Solskjaer. ***(The Transfer Window Podcast via Star)***

**FONSECA ANUKIA NEWCASTLE**

KOCHA wa zamani wa AS Roma, Paulo Fonseca mwenye umri wa miaka 48, yuko tayari kuteuliwa na Newcastle United baada Frank Lampard kujiondoa katika mbio za kuchukua mikoba ya Steve Bruce pale St James' Park. ***(Mirror)***

**EVERTON YAMTAKA SANCHEZ**

EVERTON inajiandaa kufanya uhamisho kwa ajili ya mshambuliaji wa Inter Milan na Chile, Alexis Sanchez mwenye umri wa miaka 32, huku nyota huyo wa zamani Arsenal na Manchester United akiwa huru kuondoka katika klabu ya Italia ifikapo Januari. ***(InterLive)***

**CHELSEA, NIGUEZ KIMEUMANA**

CHELSEA haitatekeleza azimio lake la awali la kumpa mkataba wa kudumu wa pauni milioni 34, kiungo wa kati wa Atletico Madrid mwenye umri wa miaka 26, Saul Niguez. ***(La Razonh)***

**DE BEEK NA MADRID**

KIUNGO wa kati wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 24, amemwomba wakala wake kufanikisha uhamisho wake wa kuhamia Real Madrid. ***(Sun)***

**SMALLING NJIA MOJA**

MLINZI, Chris Smalling mwenye umri wa miaka 31, anaweza kuwa mmoja wa wachezaji watakaoondoka AS Roma ifikapo Julai mwakani. ***(Calciomercato)***

**RUDIGER AGOMBEWA ULAYA**

KLABU ya Real Madrid na Bayern Munich kila mmoja inaamini itampata Antonio Rudiger, mwenye umri wa miaka 28, ambaye mazungumzo kuhusu mkataba wake na Chelsea yamekwama. ***(ESPN)***

**FOFANA NYOTA IMENG'AA**

NYOTA wa Leicester City, Wesley Fofana mwenye umri wa miaka 20, anazivutia klabu za Manchester United na Newcastle. ***(But! Football Club via Sport Witness)***

**LACAZETTE AZUIWA**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, atakataa ofa yoyote ya kumuuza mshambuliaji wake Mfaransa Alexandre Lacazette mwenye umri wa miaka 30, ifikapo Januari na badala yake atamruhusu kuondoka akiwa huru mara mkataba wake utakapomalizika msimu ujao. ***(Sun)***

**DEMBELE ANUKIA EPL**

KLABU ya Manchester City, Tottenham, Liverpool na Newcastle zinamtaka winga Mfaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 24, ambaye ana uwezekano wa kuondoka Barcelona msimu ujao. ***(90Min)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# DONARUMMA MAMBO YAMEHARIBIKA PSG

**Golikipa huyo anafikiria kuondoka klabuni hapo baada ya kukosa...**

**PARIS,** Ufaransa

GOLIKIPA, Gianluigi Donnarumma ataondoka Paris Saint-Germain iwapo ataendelea kutumika kama kipa namba mbili mbele ya Keylor Navas, kwa mujibu wa Calciomercato.

Uhamisho wa Donnarumma kutua pale Paris Saint-Germain ulitawala vichwa vya habari katika mji huo mkuu wa Ufaransa wakati wa kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Kipa huyo alitua Ufaransa baada ya kumaliza mkataba wake na AC Milan ya Italia na akakataa kusaini mkataba mpya na hivyo kuondoka kama mchezaji huru.

**Donnarumma alikuwa sehemu ya usajili mkubwa hapo PSG, ambao pia uliwahusisha wachezaji wakubwa kama Lionel Messi na Achraf Hakimi.**

Lakini sasa kwa mujibu wa ripoti hiyo, Donnarumma tayari anafikiria kuhusu majaliwa yake na miamba hao wa Ligue 1, kwa sababu ya kutopewa nafasi ya kucheza mara kwa mara.

Ripoti hiyo imebainisha golikipa huyo namba moja wa Timu ya Taifa ya Italia, hana furaha na namna kocha Mauricio Pochettino anavyomchukulia, kwani nia yake ni kucheza kila mechi.

Tangu Donnarumma atue hapo PSG amekuwa golikipa chaguo la pili mbele ya Navas kitu ambacho hakimfurahishi.

Tayari kipa huyo kwa sasa anahusihwa na Juventus pamoja na Barcelona ambao wanafuatilia hali yake kwa karibu.

MECHI KALI

HOME

MANCHESTER UTD

2.97 | 3.57 | 2.28

LIVERPOOL

AWAY

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom | m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO

# CHELSEA YAANDAA OFA KWA MENDY



**LONDON,** England


KLABU ya Chelsea inaandaa ofa ya euro milioni 60 kwa ajili ya kuinasa huduma ya beki wa Real Madrid, Ferland Mendy katika dirisha la usajili la majira ya baridi, kwa mujibu wa jarida la El Nacional.

Mendy alijiunga na Real Madrid akitokea Lyon katika dirisha la majira ya joto mwaka 2019 na amekuwa mchezaji muhimu katika kikosi hicho chini ya makocha walioifundisha timu hiyo.

Chelsea ni timu pekee inayotaka kumsajili mchezaji huyo baada ya majeraha ya muda mrefu yaliyomweka nje kwa kipindi kirefu, huku taarifa ikisema hatima yake bado haijajulikana ndani ya kikosi hicho.

Akiwa Real Madrid, Mendy amecheza mechi 71 huku akifunga mabao matatu na kutoa asisiti nne katika kipindi chote alichowatumikia Blancos hao.

Chelsea wanamtaka beki huyo ili kuziba nafasi zilizoachwa na Emerson aliyetimkia Lyon, huku mkataba wa Alonso ukitarajia kukamilika mwishoni mwa msimu huu.



# Arteta aanza tambo

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amesema Arsenal ilionyesha namna gani anataka icheze wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Aston Villa, hapo juzi Ijumaa.

Washikabunduki hao walipata ushindi wao wa tatu mfululizo wakati wakiifumua Villa kwenye Ligi Kuu England na kujivuta hadi nafasi ya tisa kwenye msimamo, shukrani kwa mabao ya Thomas Partey, Pierre-Emerick Aubameyang na Emile Smith Rowe katika mechi iliyochezwa kwenye dimba la Emirates.

Arsenal walikuwa mbele kwa mabao mawili kuelekea kipindi cha kwanza na kuwafanya wapige mashuti 14 katika lango la Aston Villa - ikiwa ni mara ya kwanza kuwazuia wapinzani wao kutopiga shuti langoni mwao tangu Mei, 2018 dhidi ya Burnley.

Ushindi huyo umeifanya Arsenal kufikisha mechi sita bila kupoteza kwenye Ligi Kuu England na Arteta alionyesha kuridhishwa na kiwango alichokishuhudia.

"Namna tulivyoanza mchezo na tulivyoendelea ilikuwa nzuri sana," alisema akiiambia BBC Sport.

"Tuliwashambulia kwa kasi kubwa, tulishinda kila nafasi. Tulikuwa wabunifu na tishio. Najisikia fahari kwa namna tulivyocheza. "Hivi ndivyo nataka timu icheze. Hapo ndio tunapokuwa bora, tunapocheza kwa ubora na umakini mkubwa na tunaweza kutengeneza mashambulizi.

"Tulikuwa karibu pamoja. Uamuzi wetu ulikuwa mzuri sana. Tulikuwa na wachezaji wazuri na tulicheza kwa utulivu mkubwa."

LIVE IN PLAY

# TFF YAIANDIKIA BARUA CAF

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limeandika barua kwenda katika Shirikisho la mchezo huo barani Afrika (CAF), ili kuomba kusogezwa mbele kwa mchezo wa marudiano wa mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho kati ya wenyeji Al Ahly Tripoli dhidi Biashara United ya hapa nchini.

Awali mchezo huo ulipangwa kuchezwa jana jioni, lakini TFF imeiomba CAF kusogeza mbele hadi Oktoba 27, mwaka huu ili kuruhusu Biashara United iliyoshinda mabao 2-0 katika mechi ya kwanza kufika jijini Benghazi.

**Taarifa iliyotolewa na Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo imesema shirikisho hilo kwa kushirikiana na Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo inaendelea na mchakato wa kufanikisha Biashara United inasafiri kwenda kukamilisha ratiba inayowakabili.**

Ndimbo alisema licha ya kupata ndege ya kukodi, Biashara United ilishindwa kuondoka kutokana na kukosa vibali vya anga vya kimataifa vya Sudan, Sudan Kusini na kile cha kutua Benghazi , utapochezwa mchezo huo.

"Mamlaka za Sudan, Sudan Kusini na Libya, anga zao hazifanyi kazi siku za Ijumaa na Jumamosi," alisema Ndimbo.

Mwenyekiti wa Biashara United, Selemani Mataso aliliambia gazeti hili hatima yao iko chini ya TFF ambayo inashirikiana kwa karibu na Wizara ili kufanikisha safari yao.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango (kulia), akimkabidhi mpira mwamuzi wa soka, Raphael Ikambi, kama ishara ya ufunguzi wa Michezo ya 35 ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) inayofanyika kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Mtibwa: Kagera ilituzidi mbinu*

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya timu yake kuchapwa bao 1-0 na Kagera Sugar, Kocha wa magolikipa wa Mtibwa Sugar, Soud Slim, amesema kutofuata maelekezo ndio sababu ya wao kupoteza mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba juzi.

Slim aliliambia gazeti hili wachezaji wao walishindwa kuzitumia vyema nafasi walizokuwa wanazitengeneza na kuwapa faida wenyeji wa mchezo huo ambao hawakuonyesha kiwango cha juu.

Kocha huyo aliongeza licha ya kupoteza mchezo huo, hawajakata tamaa ya kuwa kwenye mbio za kuwania ubingwa kwa sababu bado ligi hiyo ni 'changa'.

"Kagera ilijipanga vizuri, wachezaji wetu walizidiwa mbinu na mahasimu wetu mpaka ikapelekea kufungwa goli moja, kikubwa tunakwenda kujipanga kwa ajili ya mchezo ujao, tunawaomba mashabiki wetu wasikatishwe tamaa na matokeo hayo,"alisema Slim.

Kocha huyo aliongeza msimu huu ligi imekuwa na ushindani zaidi kwa sababu kila timu imejipanga kufanya vizuri katika kila mchezo ili kufikia malengo.

"Ahadi na motisha zilizoahidiwa na wadhamini wa Ligi Kuu Bara msimu huu zimechangia kuleta ushindani, nasi tutaendelea kupambana, turudi nyumbani kujipanga," Slim aliongeza.

SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA




MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 24 - OKTOBA 2021


| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:15 | 2452 | Twente vs NEC Nijmegen | 1.70 | 3.83 | 4.42 |
| 13:30 | 4636 | Atalanta vs Udinese | 1.43 | 4.92 | 6.63 |
| 14:00 | 4155 | Nice vs Lyon | 2.54 | 3.49 | 2.59 |
| 14:00 | 4534 | St Mirren vs Rangers | 7.10 | 4.44 | 1.41 |
| 14:00 | 5667 | Ufa vs Rubin Kazan | 2.96 | 3.16 | 2.38 |
| 14:30 | 4978 | Royal Antwerp vs Brugge | 3.55 | 3.80 | 1.89 |
| 14:30 | 5884 | Barnsley vs Sheffield Utd | 3.40 | 3.35 | 2.08 |
| 15:00 | 4584 | Sevilla FC vs Levante | 1.48 | 4.30 | 6.80 |
| 15:15 | 3736 | FC Luzern vs St. Gallen | 2.28 | 3.50 | 2.86 |
| 15:30 | 4146 | Cambuur vs Feyenoord | 4.92 | 4.63 | 1.53 |
| 15:30 | 5368 | Vitesse Arnhem vs GO Ahead Eagles | 1.54 | 4.34 | 5.13 |
| 16:00 | 1796 | Fiorentina vs Cagliari | 1.69 | 3.97 | 4.73 |
| 16:00 | 2514 | West Ham vs Tottenham | 2.40 | 3.41 | 2.91 |
| 16:00 | 3043 | Lens vs Metz | 1.62 | 3.97 | 5.16 |
| 16:00 | 3199 | Lorient vs Bordeaux | 2.06 | 3.43 | 3.48 |
| 16:00 | 3580 | Brentford vs Leicester | 2.61 | 3.37 | 2.66 |
| 16:00 | 4099 | Reims vs Troyes | 2.20 | 3.23 | 3.33 |
| 16:00 | 4202 | Antalyaspor vs Basaksehir | 2.56 | 3.25 | 2.66 |
| 16:00 | 5008 | Verona vs Lazio | 3.06 | 3.57 | 2.23 |
| 16:00 | 5392 | Rennes vs Strasbourg | 1.81 | 3.64 | 4.19 |
| 16:30 | 4128 | FC Koln vs Bayer Leverkusen | 3.09 | 3.83 | 2.08 |
| 16:30 | 4399 | Akhmat Grozny vs Ural Yekaterinburg | 1.75 | 3.55 | 4.54 |
| 17:00 | 1147 | Randers vs Aarhus | 2.25 | 3.30 | 3.06 |
| 17:00 | 1653 | Nottingham vs Fulham | 3.79 | 3.35 | 1.95 |
| 17:00 | 3407 | Ceske Budejovice vs Slavia Prague | 5.81 | 4.51 | 1.50 |
| 17:00 | 3434 | Dynamo Kiev vs SC Dnipro 1 | 1.30 | 5.04 | 7.94 |
| 17:00 | 5112 | Anderlecht vs Kfco Wilrijk | 1.30 | 5.53 | 7.90 |
| 17:15 | 3973 | Barcelona vs Real Madrid | 2.65 | 3.48 | 2.56 |
| 17:30 | 1282 | Pacos Ferreira vs FC Arouca | 1.95 | 3.36 | 3.80 |
| 17:30 | 5696 | FC Basel vs FC Lugano | 1.57 | 4.25 | 4.94 |
| 17:45 | 5568 | Ajax vs PSV Eindhoven | 1.43 | 4.81 | 5.89 |
| 18:00 | 4427 | RB Salzburg vs Sturm Graz | 1.26 | 5.44 | 8.36 |
| 18:00 | 4457 | Monaco vs Montpellier | 1.47 | 4.58 | 5.97 |
| 18:30 | 3848 | SuperSport Utd vs Kaizer Chiefs | 2.10 | 3.20 | 3.70 |
| 18:30 | 4718 | Stuttgart vs Union Berlin | 2.42 | 3.42 | 2.78 |
| 18:30 | 4792 | Manchester Utd vs Liverpool | 2.97 | 3.57 | 2.28 |
| 19:00 | 1474 | Fenerbahce vs Alanyaspor | 1.75 | 3.65 | 4.34 |
| 19:00 | 4317 | Zenit St Petersburg vs Spartak Moscow | 1.52 | 4.35 | 5.33 |
| 19:00 | 5421 | Roma vs Napoli | 2.76 | 3.51 | 2.45 |
| 19:00 | 5666 | Midtjylland vs Sonderjyske | 1.32 | 4.93 | 8.68 |
| 19:30 | 1306 | Betis vs Rayo Vallecano | 1.80 | 3.82 | 4.22 |
| 19:30 | 3185 | Racing Genk vs KAA Gent | 2.08 | 3.60 | 3.16 |
| 20:00 | 5161 | FC Vizela vs Benfica | 6.53 | 4.55 | 1.42 |
| 20:30 | 4138 | VfL Bochum vs Eintracht Frankfurt | 2.98 | 3.53 | 2.24 |
| 21:00 | 3190 | Groningen vs AZ Alkmaar | 4.14 | 3.65 | 1.79 |
| 21:45 | 1078 | Inter vs Juventus | 2.10 | 3.56 | 3.36 |
| 21:45 | 1432 | Marseille vs Paris St Germain | 4.46 | 4.07 | 1.68 |
| 22:00 | 2038 | OH Leuven vs St Truiden | 2.35 | 3.34 | 2.85 |
| 22:00 | 3294 | Atletico Madrid vs Real Sociedad | 1.66 | 3.74 | 5.45 |
| 22:30 | 3516 | Portimonense vs GD Estoril | 2.38 | 3.00 | 3.10 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumapili Oktoba 24, 2021

Nipashe



Donarumma mambo yameharibika UKURASA 21



Kiungo wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Enekia Kasonga (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya nyota wa Namibia, katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Dobsonville, Soweto, Afrika Kusini jana. Twiga Stars imetolewa katika michuano hiyo. **PICHA: TFF**

## Yanga, Azam FC mechi iliyojaa hesabu Bara

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Yanga umesema unaendelea kujizatiti kuhakikisha inaibuka na ushindi katika mechi yao ya raundi ya nne ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya Azam FC itakayochezwa Oktoba 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam ili kukaribia malengo yao.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Meneja wa Yanga, Hafidh Salehe, alisema wanataka kuona kikosi chao kinaendelea na kasi yake kama walivyofanya katika mchezo wao uliopita dhidi ya KMC.

Saleh alisema kila mchezaji wa Yanga anafahamu malengo waliyokuwa nayo msimu huu, hivyo kwao kila mechi ni sawa na fainali.

"Lengo letu ni kupata pointi tatu kwenye kila mchezo ambao tutacheza, kila mchezo kwetu ni fainali, hatubezi timu hata moja na tunawaomba mashabiki wetu waendelee kutupa ushirikiano," alisema Saleh.

Hata hivyo alisema wanaupa umuhimu mkubwa mchezo huo kwa sababu wanakutana na timu yenye wachezaji bora na wenye uzoefu wa mechi za kimataifa.

"Malengo yetu makubwa msimu huu ni kulibeba taji la ubingwa wa Ligi Kuu, tunajua kuna ushindani, tutapambana katika mechi zote, hatutabweteka, tunajua mbio za kuwania taji hilo si rahisi, wakati wote tutapambana ili kuipa timu mafanikio ya kweli," meneja huyo alisema.

Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea tena leo kwa Ruvu Shooting kuwakaribisha Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani na 'Maafande' wa Prisons ya jijini Mbeya itawafuata Dodoma Jiji FC kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

# Simba, Jwaneng kumaliza ubishi

## ●●● Msimbazi yatamba inataka ushindi tena na kutoa burudani kwa...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, wanatarajia kuwakaribisha Jwaneng Galaxy kutoka Botswana katika mechi ya marudiano ya michuano hiyo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Simba itashuka dimbani ikiwa na mtaji wa mabao 2-0 walioupata ugenini katika mchezo wa kwanza ambao ulifanyika mjini Gaborone wiki iliyopita.**

Kikosi cha Jwaneng Galaxy kiliwasili nchini kimya kimya tangu Oktoba 20, mwaka huu na kilikuwa kinafanya mazoezi yake kwenye Uwanja wa Isamuhyo na jana jioni kilihamia kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Thierry Hitimana, alisema wanahitaji kufunga magoli ya mapema ambayo yatawapa ushindi katika mchezo huo wa marudiano na kujihakikishia tiketi ya kutinga hatua ya makundi.

Hitimana alisema wataingia kivingine katika mechi hiyo tofauti na walivyocheza kwenye mchezo wa kwanza ugenini kwa sababu wameimarisha uchezaji na wanataka kuwapa mashabiki wao burudani huku wakifikia malengo.

"Tunahitaji kushinda lakini kuhusu idadi ya mabao hilo litafuata baadaye, kikubwa ni kupata ushindi na kusonga mbele, licha ya kupata ushindi nyumbani kwao ila hatutaingia kwa dharau, tunawaheshimu na tunatarajia kwenda kutafuta ushindi.

"Tunachoangalia kwa sasa ni kutafuta nafasi ya kuingia hatua ya makundi, tumejipanga kuimarisha kiwango cha uchezaji wetu ili kutoa burudani kwa mashabiki wetu na kufikia malengo hayo," alisema Hitimana.

Aliongeza walitumia vyema dakika 90 za kwanza kwa kutumia vizuri nafasi za mapema walizozipata, na sasa wanaingia katika dakika 90 nyingine mpya ambazo wataingia na mipango tofauti ili wasonge mbele katika michuano hiyo.

Nahodha Msaidizi wa Simba, Shomari Kapombe, alisema wamejipanga vizuri kukabiliana na Jwaneng Galaxy huku wakiwa wameondoa kichwani matokeo walioyapata walipokuwa ugenini Botswana.

Kapombe alisema wanaimani wapinzani wao pia watakuja kivingine, licha ya kucheza nyumbani wanakuja kivingine kwa kuanza upya mchezo huo na kutafuta ushindi ili kupata nafasi ya kuingia makundi.

"Tumejiandaa kufanya vizuri na tunatambua wapinzani wetu hawatakuja kama walivyokuwa kwao, ila hawatapata nafasi kuharibu rekodi yetu, tutahakikisha tunaendelea kutumia vyema uwanja wetu wa nyumbani," alisema Kapombe.

Aliongeza wachezaji wote waliokwenda Botswana wako fiti na tayari kwa mchezo huo wa marudiano ambao wamejipanga kuwapa burudani mashabiki na wanachama wao.

Wakati huo huo, Nipashe jana ilishuhudia kiungo mshambuliaji wa Simba, Pape Ousmane Sakho akirejea katika mazoezi pamoja na wachezaji wenzake baada ya kupona jeraha la mguu lililokuwa linamsumbua.

Daktari wa timu hiyo, Yassin Gembe, alisema uwezekano wa nyota huyo kuwapo katika kikosi kitakachocheza mechi ya leo ni mdogo kwa sababu hajawa fiti kwa asilimia 100.

Simba imeanzia raundi ya kwanza baada ya msimu uliopita kutolewa kwenye hatua ya makundi na endapo itashindwa kusonga mbele katika michuano hiyo, itahamishiwa kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >